



(CKRC)

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED] **VERBATIM REPORT OF** [REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

MALAVA CONSTITUENCY,

HELD AT SHAMONT SECONDARY SCHOOL

7TH AUGUST 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MALAVA CONSTITUENCY, HELD AT SHAMONI
SECONDARY SCHOOL 7TH AUGUST 2002**

Commissioners Present

Zein Abubakar - Commissioner
Mosonik Arap Korir - Commissioner

Secretariat

Hassan Mohamed - Programme Officer
Joyce Wamucii - Ass. Programme Officer
Marion Nekesa - Verbatim Recorder.

The meeting started at 9.30 a.m.

Co-coordinator Mr. Caleb Amaswache: Watu wa Kabras division kwa jumla hamjamboni. Mbele yenu ni Macommissioners kutoka katika tume ya kurekebisha katiba. Tulichagua station ya Shamoni tukae hapa kidogo kwa sababu tuliona nyinyi kutoka hapa kuja Malava ni mbali sana, halafu tukasema tulate huduma karibu na nyinyi. Kwa sababu tunajua trend vile watu huwanga wanakuja kwa hii mkutano hatuwezi tukangoja tukasema kila mtu akuje. Tutaanza mkutano na kabla hatujaanza, jina langu ni Amaswache Caleb Themba mimi ndio co-coordinator wa Malava na Lugari. Tutauliza mmoja wenu atuombee halafu mkutano uanze. Asanteni.

Maombi: Baba wetu katika jina la Yesu Kristo tunakuinua na kushukuru ya kwamba ni asante kwa vile wewe mwenyewe ulipanga siku hii ya leo ili tukuje hapa tuzungumze mambo ya kujenga nchi yetu. Yesu mwana wa Mungu wale ambao wameingia hapa nawakabidhi wote mikononi mwako na wale ambao wangali njiani tembea na wao ili tushirikiane tuwe kitu kimoja. Tukianza tutaanza na wewe tena tukimaliza tumalize na wewe naomba nikiamini kwa upendo wa Yesu Kristo ndiye Bwana wetu. Amen.

Co-coordinator Mr. Caleb Amaswache: Kidogo nilukuwa nimesahau kuwaambia kuna mwenzangu mmoja mwenye ananisaidia, my assistant is outside there, his name is John Karouki yeye ndiye anaandikisha watu hapo nje. Asanteni Commissioners welcome, I hand over the meeting to you.

Com. Zein Abubakar: Eeh, habari ya asubuhi. Jambo langu la kwanza ambalo ninafaa kutenda ni kukitambua kikao hiki kama kikao rasmi cha tume ya kurekebisha katiba kwa minajili ya kupokea maoni ya Wakenya ili kubadilisha katiba yetu. My first duty is to recognize this as an official and formal sitting of the constitution of Kenya Review Commission, for the purpose of collecting views from Kenyans to amend our constitution. Nikisha kitambua namna hio kinakuwa kikao rasmi sasa cha tume ya kurekebisha katiba.

Jambo la pili ningemuomba Commissioner ambaye amekaa mkono wangu wa kushoto ambaye tutafanya naye kazi pamoja, awaambie na ajitambulishe kwenu halafu tutaendelea.

Com. Dr. Mosonik Arap: Hamjambo wananchi wa Malava. Jina langu ni Mosonik Arap Korir ni Commissioner. Asanteni.

Com. Zein Abubakar: Asante sana Dr. Mosonik. Mimi naitwa Abubakar Zein na mimi pia ni Commissioner katika tume ya kurekebisha katiba. Hivi leo sisi wawili ndio tutakuwa tunasimamia kikao hiki na kuchukua maoni yenu. Tulikuwa kama tume tumegawanywa katika vikundi vitatu, vya commissioner watatu watatu. Na commissioner watatu ambaye angekua nasi hapa leo ni Commissioner Isaac Lenaola lakini alihitajika kurudi katika makao yetu makuu huko Nairobi kwa mambo ya kazi ya tume, na alienda huko. Sasa sisi leo tutakuwa tunasimamia kikao hiki.

Tume imesanya maoni ya Wakenya nchi nzima, na leo ndio tunamalizia hapa kwenu, na leo itakuwa siku ya mwisho ya kukusanya maoni. Tutakuwa tukimaliza hivi leo, tutakuwa tumekamilisha kukusanya maoni katika sehemu za uakilishaji bungeni mia mbili na kumi. Na nyinyi kuwa ni watu wa mwisho au watu wa kufunga kikao si kwamba mnavuta mkia, nyinyi mlibahatika kuwa na nafasi bora ya kujitayarisha na kuwa na fursa ya kihistoria kwamba nyinyi ndio mtafunga vikao vya tume vya kurekebisha katiba katika kukusanya maoni. Kuna vikao vingine vya tume ambazo vinaendelea leo. Kuna kikao kule Emuhaya, kuna kikao Hamisi, kuna kikao Budalang'i, kuna kikao kingine, Khwisero, Ikolomani na Matungu pamoja na hichi kikao cha leo. Ikifika jioni tutakuwa tumefunga vikao vyote, na tutakuwa tumemaliza kazi ya kukusanya maoni katika sehemu za uwakilishaji bungeni na tutakwenda kutayarisha maoni hayo kama baada ya wiki tutakuwa tumemaliza kazi ya kutayarisha na

kuyasikiza maanake kazi ya kuyatayarisha yanaendelea. Tulikuwa tunafuatia alphabetical order ya Kiingereza, kwa hivyo tulianza na Central province, tukaenda Coast province, sasa tunamalizia Western. Ndio ya misho katika mikoa.

Jambo lingine la muhimu mimi kuwaambia ni kwamba leo ni siku muhimu sana, na sina haja kusema sana kuhusu hayo kwa sababu nyinyi mnafahamu ndio mko hapa. Sasa kiasi tunamsubiri Mkuu wa shule afike maanake mila na desturi zetu za Kiafrika hazituruhusu sisi kuanza mambo bila mwenyeji wetu kuweco, yeye ndio Mkuu wa shule. Karibu nilikuwa nimetumana uitwe.

Nilikuwa nazungumzia kuhusu kwamba leo ndio tunamaliza vikao vya tume na ningependa kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Principal kwa kutupa fursa sisi kuja katika shule hii, na kutumia Hall la hapa kufanyia kazi hii muhimu. Na kumweleza tu kwamba bwana Principal jambo hilo nzuri mliofanya ni la kihistoria kwa sababu tutakapomaliza kazi zetu, tutachapisha watu wote waliochangia pamoja na tasisi zilizochangia kufanya kazi yetu ikawa imefana. Na nyinyi mtakuwa katika ile roll of honour, tutakuwa na roll of honour na shule yenu itakuwa katika roll of honour na ninafurahi kwamba pia umetayarisha wanafunzi ambao wako hapa wengine watatoa maoni kwaniaba ya wanafunzi wengine; na tungeomba tukupe fursa hii najua tumeshavunja mipaka ya kuwa wageni, chukua fursa hii utukaribishe rasmi. Asante.

Isiah Luchiko Kakai: Wageni wetu wa siku ya leo, wananchi ambao wamefika ningependa kuchukua nafasi hii niwakaribisheni katika shule ya upili wa Shamoni kwa jambo hili muhimu; kikao ambacho ni cha manufaa sana kwa taifa nzima la Kenya. Kabla hatujaendelea sana ningesema kwa vile(?) tuko katika harakati ya kukamilisha terminal reports na baadhi ya wanafunzi tulionelea wasiwe hapa wengetupigia sisi makele makae nyumbani, na wale ambao wamejiandaa kutoa maoni yoa wachangie katiba ya Kenya, na nawatarajia nadhani wako karibu kufika.

Tuna waalimu wachache na tuna wanakijiji, na mimi binafsi kwa majina ni Isiah Luchiko Kakai, ningependa kusema kwa niaba ya shule na halmashauri ya shule ni kwamba tumepokea tumeheshimu,(?) mumetuchagua kuwa kuchangia katika kupeana hii Hall(?) na tunachukua vizuri tunachulia mvua.....(?). Kwa hivyo mkiwa hapa mjisikie mko nyumbani. Najua tatizo liloko Africa ni kwamba watu hawazingatii wakati, lakini nina hakika kuwa wananchi watafika, na watachangia vizuri viwezekanavyo. Asante sana.

Com. Zein Abubakar: Asante sana bwana Principal tunashukuru kwa maneno yako pamoja na ukarimu wenu wa kutukaribisha hapa. Sasa mimi nitaanza tu kwa kutaja mambo yaliyo muhimu ili tufahamikiane katika kutoa maoni yetu ili tuwe na nidhamu pamoja na kuendesha kazi hii inavyotakikana.

Kwanza kabisa, kila Mkenya anayeingia hapa anahitajika kujiandikisha nje pale. Hata kama utakuwa hutoi maoni, umekuja tu kushuhudia mambo yanayo tendeka hapa; pia unahitajika kujiandikisha pale. Na ukijiandikisha pale itaandikwa kwamba wewe ni observer au ni mtu uliokuja kushuhudia au kuwa shahidi kwa mambo yanayotokea hapa.

Kwa hivyo ningepomba wale ambao hawajajiandikisha nikimaliza kutoa mwelekeo huu, waende pale nje wajiandikishe.

Pili kwamba ikishajaa form ambayo zile zinaendelea kuandikiswa pale tunaweza chelewa sisi. Kama sasa tuna form mbili tayari, na hii form ndio tutakayotumia katika utaratibu wa kuita majina ya watu ili waje watoe maoni. Yule aliyejiandikisha jina lake kwanza ndiyo atakayepewa fursa ya kwanza kuzungumza. Lakini sisi kama tume tulikuwa tunajipa haki na kuwaomba nyinyi mtupe haki hio ya kutoka katika utaratibu huo ikiwa kuna sababu za kutosha lakini si kwa muda mrefu halafu tutarudi kwenye utaratibu. Na baadhi ya sababu ambazo zinaweza kutufanya sisi kutoka katika utaratibu huo, ni kwamba tuwe na mwalimu ambaye pengine ana kazi za kusahihisha mtihani kama alivyosema Principal, na angeomba apewe fursa azungumze halafu ndio arudi kwenye kazi hiyo; tutaomba nyinyi utupe haki hiyo, kumpa mwalimu kama huyo haki ya kuzungumza halafu aende. Au akaja mama mjamzito ambaye hawezi kuvumilia kukaa kwa muda mrefu, pia tunaomba haki hiyo hiyo. Au akaja mtu mlemavu, au mtu mzee sana yaani ni watu ambao kawaida sisi kabila zetu za kiafrika huwa tunawafikiria. Sijui kama mnatupa haki hiyo, eh sawa eh.

Jambo lingine la muhimu kufahamu ni kwamba, sisi tumetoa njia tatu za kutoa maoni. Njia ya kwanza ni kwamba uwe na maandishi, au memorandum; eh umetayarisha maandishi yako kwa muda mrefu, unayo sasa na unataka kutupa sisi kama tume. Hiyo njia ya kwanza inaweza kukufanya wewe ukaenda moja moja kutoa maandishi hayo kwetu. Na tutatumia njia ya, najaribu kufupisha nazungumzia hivyo kwa kazi pamoja na kuwajulisha kwenu, wafanyi kazi wa tume tuliokuja nao, niwajulishe halafu nirudi tena niwaambie kazi zao; lakini nataka nikiwaambia kazi zao ndio mtawakumbuka vizuri. Sasa nitaanza na yule bwana aliye kaa pale yule. Yule ndio kiongozi wa wafanyikazi wa tume tuliokuja nao anaitwa Hassan Mohammed, Hassan Mohammed ni Programme Officer katika tume ya kurekebisha katiba ya Kenya. Ukiwa unamaandishi yako na wewe hutaki kuzungumza sijui kama tunaielewana, una maandishi hutaki kuzungumza unataka kutupa tu maandishi hayo sisi tuyashugulikie uende moja kwa moja baada mimi kumaliza mazungumzo, unaweza kuenda moja kwa moja ukatole maandishi yako kwa Programme office, ambaye ni kiongozi na msimamizi wa kazi za leo. Atayachukua na uta sign register yetu baada ya kwamba umejiandikisha kwa hii form utasign kwenye register tofauti ya form hii, na register ile ni kwamba register ile inasema kwamba wewe umetoa maoni, form hii inasema wewe umehudhuria kikao. Unaona register aliyoinua utasign hapo, halafu ile memorandum ulioleta utamwachia ukaiweka katika file ile. Kila kikao kina file yake, kwa hivyo kikao cha hapa Shauri Moyo itakuwa file yake ni hii. Utatoa utakuwa unemaliza kazi, ukitaka utakaa chini usikize wenzako, au ukitaka utakwenda nyumbani. Hilo limeeleweka, hiyo ni njia ya kwanza.

Njia ya pili ni kwamba unamaandishi una hiyo memorandum, lakini huitaki kutoa hivi hivi unataka upewe fursa uchague yaliyomuhimu katika memorandum ile, uyazungumzie ili Wakenya wengine wajue ni mapendekezo gani unatoa kwa tume ya kurekebisha katiba. Hiyo ndio njia ya pili, unaruhusiwa hivyo. Na ukija hapo tutakuomba usisome yote kutoka mwanzo mpaka mwisho. Utuchagulie na utuchambulie yaliyo muhimu, na useme Wakenya wenzangu, haya ndio mambo muhimu ninayoyatoa kwa tume. Na njia hiyo ya pili tutakupa dakila ngapi? Tano, uzoefu wetu wa kazi unatuonesha kwamba ukitumia dakika tano zile, kutoa mapendekezo na mambo muhimu, zinakutosha kabisa. Kuna njia ya tatu, hii njia ya pili imeleweka? Eh.

Njia ya tatu, njia ya tatu inasema hivi; kwamba wewe unataka kutoa maoni yako kwa mazungumzo, kwa kauli yako utoe yaliyo moyoni na kichwani kwa ulimi wako bila kutoa maandishi. Pengine una maandishi kidogo ambayo umeandika points tu zikukumbeshe jinsi tutakavyozungumza hiyo pia inakubalika. Sisi tungependa kutoa dakika tano pia kwa mtu kama huyo lakini kwa vile atakuwa hajaandika maoni yake, ikiwa bado unatoa points ambazo zinahusiana na ubadilishaji wa katiba, tutakuongezea muda, up to ten minutes, lakini haipiti dakika kumi. Sijui kama tunaelewana. Nitakujaribu kukuweka kwenya line ya dakika tano, lakini up to ten minutes, kwa sababu utakuwa pengine unayakumbuka kwenye akili. Ni sawa hivyo au si sawa? Maanake sisi hujaribu kuwaomba watu tukubaliane maanake ukiseme tumpe mtu two hours, tutashauriana halafu tusema ni sawa, halafu wazungumze watu wachache. Hizo ndio njia tatu.

La muhimu pia kuelewa kuhusu maneno unayozungumza hapa ni kwamba, commissioner mwenzangu na mimi, tunaandika kwa mkono. Mnavyosema pengine tunasikiza halafu tunaandika yale tunaona tunafaa kuandika. Halafu kuna yule binti amekaa pale, ameinua mkono anaitwa Joyce Wamucii. Jocye, kazi yake yeye ni assistant programme officer, na atakuwa akiinukuu akiandika kwa mkono mambo yote yanayotokea hapa. Nani akasema nini, nani alianza vipi, yote anaandika kwa mkono. Halafu kuna yule binti amekaa pale, anaitwa Marion Nekesa, Marion Nekesa ni verbatim recorder, unaona amekaa karibu na speaker na ana tape zaidi ya moja, hiyo moja anaonesha mifano kwa sababu ile ingine inaendelea na kazi kule. Kazi yake yeye ni kurecord kila neno linalosemwa hapa.

Wengine wanasema hata ukikohoa, kikohozi chako kitakuwa mle ndani. Kwa hivyo usiwe na wasi wasi maneno yako pengine yatapotea, commissioner mwenzangu au mimi tumesita hatuandiki tunakusikiliza tunataka kukuelewa, kusema mbona hawaandiki mambo yangu muhumu ninayosema? Tunarekodi tatu ya macommissioner, ya binti Jocye, na binti Marion anarekodi kwa record, verbatim recording. Sijui kama tumeelewana. Hatutaki kitu chochote kipotee, ni sawa hivyo?

Sasa tuzungumze mambo ya lugha. Lugha ambayo tutatumia hapa ni Kiswahili, ambayo ndio lugha yetu ya taifa, Kiingereza ambayo pia ni lugha rasmi nchini. Kuna mtu yeyote asiyejua lugha hizo mbili? Kusema tunasema hivi, ikiwa wewe unajiamini kwamba mambo wawili, ikiwa kwanza hujimudu kuzungumza Kiswahili au Kiingereza, una haki ya kutumia lugha ye yote ingine ya Kenya, ambayo inazungumzwa na watu wengi hapa. Ni lugha gani inayozungumzwa na watu wengi hapa? Kiluhya cha aina gani? Eh Ki Kabras ndio unaweza tumia ukiwa unataka, hio ni njia ya kwanza, kama humudu Kiswahili au Kiingereza.

Njia ya pili ni kwamba pengine unamudu Kiswahili na Kiingereza lakini kuna mambo mengine unasema huwezi kuyaeleza isipokuwa kwa Kikabras. Lakini tungewahimiza wengi wenu mtumie Kiswahili na Kiingereza ikiwa unaweza kukimudu na unaweza kujieleza ya kutosha. Kwanini tunasema hivyo? Kwa sababu ikiwa tutatumia Kikabras utatakiwa mtu wa kutafsiri awekwe hapa ukizungumza halafu yeye anatafsiri, kwa hivyo atachukua nafasi za watu wangapi? Wawili. Hatusemi usitumie, unahaki hio, lakini utumie kwa kuwa unawatilia manani wenzako pia wanataka kutoa maoni, au si sawa hivyo?

Haya, kuhusu lugha tena, lugha tutakayotumia hapa, ni kule kwetu Mombasa tunasema lugha murua, lugha yenye heshima ambayo haitakufanya wewe ukasirike, ikiwa ni mzee amekuja mtu akazungumza hapa hautakasirika, ikiwa ni kijana hautakasirika, ikiwa ni mtoto hautakasirika. Lugha ambayo inaheshimu kila mtu.

Halafu, ni muhimu sisi kukuambia pia lolote utakalosema hapa unalindwa kisheria. Sheria inavyotulinda sisi, ndio inawalinda ninyi. Hakuna mtu atakayekufuata au tahsisi itakayokufuata kuuliza kwanini ulitoa maona haya? Unalindwa kisheria. Lakini kwamba unalindwa kisheria isitumike kwamba hiyo ni fursa ya kugeuza kikao hiki kuwa kikao cha fujo, hatutakubali mtu kuja kutukana mwingine, kumharibia jina au kutaja watu majina.

Ukiwa wewe una matatizo na Commissioner Abubakar Zein wacha nijifanye mimi ni mfano unamatatizo na mimi zungumzia ofisi ya commissioner usinitaje mimi jina. Sijui kama ni sawa hivyo eh? Ukitaka kuzungumzia ofisi ya chief ni sawa; lakini usije ukasema, mimi na chief fulani tuna matatizo yetu nyumbani uanze kutuambia habari ya matatizo yako na huyo chief umemtaja. Unaweza kutaja kama una matatizo na chief lakini usimtaje jina. Ni sawa hivyo.

Lingine la muhimu kabisa kufahamu ni kwamba, tunaomba mtakapokuwa mkitoa maoni unaweza kuzungumzia shida na matatizo tuliyonayo kama Wakenya, na shida hizo na matatizo Wakenya wengi wanazijua; lakini la muhimu zaidi ni wewe kutupa mapendekezo, je tutatia nini, ni mambo gani katika katiba mpya. Ukituwacha na matatizo peke yake, itatupa sisi kazi ya kuenda kukutafutia njia ya kutatua na pengine haitakufurahisha. Ikiwa unazungumzia elimu, utuambie unataka vipi. Ikiwa unazungumzia uchumi, utawala, viongozi, kila kitu uzungumzie ukituambia nataka hivi na hivi.

La mwisho kabisa, mambo mawili ya mwisho. La kwanza ni kwamba, nitaomba ninyi mnipe ruhusa mimi kwa sababu nimepewa fursa na ndugu niwe Mwenyekiti wa kikao hiki leo. Ikiwa mtu ametoka kwenye line anazungumza mambo ambayo hayahusiani na ubadilishaji wa katiba nimrudishe kwenye line, mnanipa ruhusa hivyo, nimwambie ndugu rudi kwenye line.

La pili, ni kwamba sisi tuna mila ada na desturi kama waafrica. Na mila na ada na desturi zetu zina heshima; na kawaida mtu akipewa fursa kuja kuzungumza huanza na kusema, ma commissioner mlifika hapa hivi leo, tunawakaribisha sana, tunawapongeza kwa kazi nyingi mnayofanya watusifu kidogo si ni kawaida hii? Wamtaje na pincipal, na chifu wetu akija, akaja mbunge utamtaja na mbunge wetu, na viongozi mbali mbali wa kidini. Achukue dakika tano zile tulimpa kutukaribisha. Na hiyo ndio mila na desturi yetu, na kwamba katika mila zetu mtu ambaye amekomaa kimawazo, hawezi kuendelea kutaja jambo moja kwa moja, lazima azungumze kwa kuzunguka au sio hivyo? Si ni hivyo, lakini ningewaomba leo mila, ada na desturi hiyo tubadilishe, kwa leo tu.

Ikifika jioni tutarudi kwa mila zetu, ni nzuri. Lakini kwa leo ukija hapa, ukishaitwa jina unakuja hapa unasema, mimi jina langu fulani wa fulani. Sio kwamba hatujui jina lako, tumekuita; tunataka sauti yako wewe mwenyewe itaje jina lako wewe mwenyewe kwa kujitambulisha. Useme mimi fulani wa fulani. La pili utakalofuatia, mapendekezo yangu ni haya. Sijui kama

mnafahamu hayo.

Na ikiwa ni mwanafunzi, mwanafunzi kidogo pengine tutatoka katika ada hio na tumwambie atutajie jina lake darasa lake, shule yake, ma miaka yake. Na ikiwa unawakilisha kikundi, tutakuambia ututajie jina lako, na jina la kikundi chako. Ni sawa hivyo? Bwana coordinator, tunahitajika kuwa na mtafsiri wa ishara, sign language interpreter. Yaani kukiwa ndugu yetu ambaye hasikii ataweza kufuatilizia mambo yanatokea katika kikao hiki kupitia ishara. Ameenda kuitwa yuko karibu kuja.

Na Caleb Amaswache ambaye ni co-coordinator atakuwa anatafsiri kwa Kikabras. Ikiwa kuna mtu anataka kuzungumza Kikabras. Na ikiwa kuna mtu yeyote anataka usaidizi, tafadhali usije kwenye meza hii, uende pale kwa programme officer utoe malalamiko yako, au uombe usaidizi wako, halafu yeye atajua jinsi ya kushughulikia ombi lako.

La mwisho kabisa ili tuanze, ukiwa uko katika kikao hiki, unajua nilianza kwa kusema kikao hiki ni kikao rasmi cha tume ya kurekebisha katiba. Mtahitaji kuwa na mkimia kabisa. Sijui kama tunaielewana. Tuwe completely silent, hata silence iwekwe hapo, kwamba atakaye ruhuswa kuzungumza ni aidha sisi tuko hapa, au yule atakayekuwa akizungumza pale. Ukiwa upande ule unataka kuzungumza na rafiki yako, utoke nje mzungumze, mmaalize, mrudi ndani ilikuheshimiana maoni ilikuheshimiana maoni. Ikiwa kuna jambo atakalosema mtu, litakukasirisha au litakufurahisha ubaki nalo moyoni mwako. Likiwa litakufurahisha ukapiga makofi na kushangilia, likikukasirisha utafanya nini? Utasomea, eh bas hapa kuwe kimwa kabisa hakuna makofi leo, ada hiyo ya makofi tumeondoka nayo, hakuna makofi, hakuna kushangilia, hakuna kukasirika. Ikiwa hukubaliana na jambo, ngoja fursa yako ikija, useme sikubaliani na jambo hili. Ukiwa unaunga mkono, ngoja nafasi yako ije, muunge mikono.

Sasa la mwisho kabisa mimi nauliza je, kuna mwenye swali kuhusiana na haya niliyosema, eh? Si mambo ya civic education ama swali mengine; kwa haya niliyoyawapa kama muongozo, kuna mtu yeyote mwenye swali? Hakuna, kuna mtu yeyote ambaye hukubaliani na muelekeo huu tuliyotoa? Hakuna, kwa hivyo naomba nipe fursa ni mwrite mzungumuzaji wa kwanza aliyebahatika kutufungulia kikao chetu leo, ni Benard Wako Wanjila. Na ikiwa nitataja jina la matu vibaya ni kwa sababu ya kuandikwa kwake, au ni kwamba ulimi wangu huajazoea kutaja majina ya aina hio, na utanisamehe kwa mwanzo, asante sana.

Benard Mwaka Wanjila: Kwa majina yangu ni Benard Mwaka Wanjila. Wa Kabras Emirembe, mimi niko na maoni yafuatayo na kwanza ni kuhusu rais, ama the presidency in this country. Mimi ningependa kupendekeza ya kwamba, rais wa nchi hii hutilia manani makabila yote ya nchi hii. Kufuatana na hayo, urais uzunguke katika mikoa ya Kenya yote, kwa kipindi cha miaka kumi kwa kila mkoa. Na mkoa wa Nairobi kwa sababu ni mji mkuu wa Kenya, tutengewa makabila ambayo ni machache sana kama Wahindi na Wazungu wawe considered wakati mkoa wa Nairobi unafikiwa.

La pili ni kuhusu utawala wa mikoa, ama provincial administration, hii ningependa kupendekeza ya kwamba idumishwe iweko lakini wapewe mamlaka na elimu zaidi, ili washughulikie maswala kama ya kulinda mazingira, environmental conservation; na kilinda haki za watoto na kuelimisha watu wakati kuna majanga kama ya magonjwa kama ya ukimwi, na shida zingine za

kawaida. Lakini wapewe mamlaka ya kushurutisha watu kuungana kufanya kazi kama kurekebisha barabara na kazi zingine kama hizo.

La tatu ni hizi pombe za kienyeji, ama local brews. Mimi ningependa kupendekeza ya kwamba serikali ya Kenya, iruhusu wananchi ya Kenya kutumia pombe zao za kiasili; kama hapa busaa, changaa na zingine. Na kama serikali inataka kusimamisha pombe, hata beer isiruhusiwe kunywewa Kenya kwa sababu hio ni pombe pia.

La nne ni administration of justice, hapa Kenya ukishtakiwa ama ukishtaki mtu, kesi inachukua muda mrefu sana, hata unaweza kushindwa kumaliza kesi. Kesi zifanyike kwa haraka kuwe na courts kwa kila divison, na kuwe na muda ambao kesi itafanyika. Na mimi napendekeza kesi isichukuwe zaidi ya miezi minne.

Kuhusu sheria ya nchi, ama land matters, hapa Kenya kununua shamba ama kurithi, ama kupewa inakuwa bei ghali sana kupata title deed. Hii inatakikana kurahisishwa na watu wapewe vieti vya kumiliki mashamba na DO, na chief, village elders wapewe mamlaka kumaliza maneno ya mashamba, bila watu kupelekwa mbali na kutumia pesa mingi, na vile mambo yalivyo sasa.

Kuhusu ndoa, maneno ya kuoja, sisi Waafrika kutoka zamani mtu anaruhusiwa kuoja zaidi ya mke mmoja. Hii iwekwe katika sheria yetu, kwamba mtu akiwa na zaidi ya mke mmoja, apewe marriage certificate. Isiwe eti mke mmoja ndiye anatambuliwa, hii ni tabia ya Kizungu, ni ya kigeni, na sisi tunaumia sana hapa kwa sababu ya hiyo. Nikiwa na wake zangu watatu, wote wapewe marriage certificate na watambuliwe sawa kama wake zangu.

Kuhusu watoto, sheria hii mpya, inatakikana iwe sheria kwa serikali kutunza watoto wote waliozaliwa katika nchi. Na mtoto atambuliwe kutoka siku mwanamke amepata mimba, kwa sababu huyo ni mtoto. Na mwanamume akifanya mwanamke mimba, na asiitunze mtoto achukuliwe sheria, afungwe afanye kufanyia serikali kazi na serikali itunze watoto wote. Katika sheria mpya ningependa kuona watoto wote ambao wako barabarani wanaitwa street children waondolowe wawekwe mahali, watunzwe na serikali wapewe elimu, wapewe chakula na malezi bora. Hilo ni jambo la muhimu sana kwangu na ninaumia sana kila mara nikiona watoto wanavuta glue kwa barabara, na wanalala kwa barabara; hiyo hianifurahishi hata kidogo.

Kuhusu local councils, hizi local councils inatakikana councillor wote wawe watu wa elimu ya form four. Hii ni kwasababu saa hii tuko kwa age ya computer na internet, na elimu imeenda juu na tunataka councillor wawe able kuelewa mambo ya kisasa, waende seminars hata akienda ng'ambo asikie ile maneno inayoendelea huko na atuletee. Kwa hivyo wawe na elimu ya kutosha.

Kuhusu taxation, ama ulipaji wa ushuru; saa hii serikali mwongozo ile inatumia kutax Kenyans si nzuri. Mimi napendekeza ya kwamba wale watu ambao wanabiashara ndogo ile ina capital ya chini ya shilingi elfu moja, wasilipe ushuhuru; kwa sababu hao ni watu ambao wanajaribu kujimudu kimaisha, na hii wakati wanafukuzwa na watu wa county council kulipishwa ada, hio inaua

biashara na inaua uchumi. Kwa hivyo taxation, watu wakiwa na vitu kidogo ya shilingi elfu moja, wasilipe ushuhuru.

Kuna hii jambo la registration of societies katika nchi, hili haswa nalenga upande wa makanisa. Katika sheria ya nchi sasa, ni vigumu sana Mkenya kuregister society haswa ya kidini. Kwa sababu wameweka sheria kali, na sisi tunaona mtu akitoka nje, kama mzungu akiwa hapa akiwa na organization yake, ni rahisi sana kuregister kuliko sisi wa Kenya.

Makanisa yawe treated kama companies, hata zikiwa milioni moja, wananchi ya Kenya wepewe uhuru wa kujiandikisha vyama na makanisa, vile wanataka; isiwe na restriction yeyote.

Na mambo ya afya ningependa kupendekeza ya kwamba serikali isisema, tusiambiwe tu ati kuna free medical care, serikali ihakikishe ya kwamba kila health centre iko na madawa na hata kama ni kuincrease taxation kwetu sisi wa Kenya, tulipe ushuru zaidi ili tuwe na matibabu kwa kila Mkenya. Na kuna magonjwa ambayo ni bei ghali sana kutibu, kama ugonjwa wa cancer, ugonjwa wa diabetes, na huu ugonjwa wa ukimwi. Serikali katika katiba hii lazima iweke mkazo ya kwamba, kila serikali itakayokuja kwa nchi; lazima itoe madawa bure, na utunzaji kwa wale wagonjwa wa cancer, ukimwi, na yale magonjwa ambaye yanahitaji pesa mingi ili kutunza wagonjwa wa ugonjwa huo wa cancer na ugonjwa wa moyo.

Kwa upande wa security, mimi ningependa kupendekeza katika katiba mpya, all security agents kama polisi, wasiwe na mapendeleo katika kuapply the law. Kwa sababu tumekuwa tukiona polisi kama watu wa upinzani wakiwa na rally yao hawatoi usalama, ama wanatumiwa kupiga watu. Hii sio kazi nzuri. Na katika katiba hii, polisi watengwe kabisa na siasa, na vyama vya utawala. Wasiongozwe na mwanasiasa, kwa sababu kuna wa Kenya ambao hawalindwi kabisa na polisi wakati mwingine; kwa sababu labda ni mpinzani. Hiyo tunataka katika katiba mpya iondolewe. Na commissioner wa polisi ama askari yeyote ambaye anasimamia area fulani akiwacha watu waumize mtu fulani achukuliwe hatua na sheria. Na ningependa kuhusu upande wa security; kuna sehemu katika nchi ya Kenya ambazo hazikaliki, na kuna majeshi Kenya, kuna GSU, kuna navy, kuna askari wengi sana hapa nchini. Hizo sehemu ambazo zimekuwa declared security zone, wapeleke huko majeshi kisheria, mpaka kila sehemu ya Kenya iwe huru kwa Mkenya yeyote kuishi na kufanya kazi na kufanya biashara.

Kwa upande wa social services, huduma ya kijamii, upande wa michezo; serikali kupitia katika katiba mpya, ningependa kupendekeza ya kwamba kuwe na pesa maalum: zipewe kwa kila area ya councillor location. Ili wapromote michezo, mbio na mipira na kila aina ya michezo, ili kuzuia vijana kujiingiza kwa maneno ya uhalifu.

Na upande wa mishahara ya wafanyikazi wa serikali, wabunge macouncillor na hata Rais. Ningependa kupendekeza ya kwamba mishahara yote ya Kenya iwe ikitengenezwa na Public Service Commission. Tusiwe na wakati kama sasa tumeona wabunge wanajiamulia mishahara yao wenyewe, na hii inatufanya sisi Wakenya wengine tujisikie kama tuko discriminated. Na hata retirement benefits kama vile walikuwa wakifanya za rais wetu ambaye ana retire sasa; tunataka hiyo package iwe tailored, iwe sawa na Mkenya mwingine yeyote ambaye ana serve katika public. There should be no special treatment for any Kenyan,

because that amounts to discrimination, we want all Kenyans to feel the same to be given equal treatment.

Interjection Com. Zein Abubakar: Umemaliza dakika zako na wewe una memorandum
.....(Inaudible)

Benard Mwaka Wanjila: Unisamehe. Sasa ningependa kwa upande wa international relations, Kenya imekuwa ikisign mikataba ambayo unasikia sheria ya watoto nini nini, hizo vitu zote ziko katika mila na desturi zetu. Wakati wanataka kusign mikataba hiyo, washauriane na sisi, kupitia kwa bunge; ili sisi tuhusike katika mikataba mengine. Kwa sababu mengine inatumiza ama ina interfere na cultural beliefs zetu.

Management ya natural resources, wale watu ambao wanashikilia ofisi za umma lazima wadeclare their wealth, na vile amepata kwa sababu tunataka tuongoze*end of side A tape I* Kwa sababu kuna watu ambao kutokana na matendo yao, hawawezi kukaa kwa watu. Na kutumia pesa kwa serikali tena kuwatunza si vizuri, kwa hivyo mtu anyongwe kama amefanya makosa makubwa, eh yale yanalingana na hiyo makosa yake.

Ya mwisho ni transfer of power, yaani kutoka rais mmoja hadi mwingine. Mimi ningependa kupendekaza ya kwamba wakati wa uchaguzi kama president ambaye ako kwa ofisi anagombea kiti, asiwe rais tena yeye ana campaign anataka kuwa president.

Speaker wa bunge awe acting president wakati president ambaye aka kwa ofisi anaenda kuuliza wananchi tena wampe nafasi ingine.

President akisha staafu aishi kama raia, asiandikiwa maaskari wapishi, yeye pia alipe watu mshahara, ajiri watu na awalipe na pesa zake. Asante sana.

Com. Zein Abubakar: Swali langu moja tu linalohusiana na maraisi wanaostaafu, viongozi wanaostaafu, wewe unapendeza mambo mawili. La kwanza unasema kwamba awe na marupurupu kama watu wengine tu. Asiwe na magari na security, na umeongezea la pili hapo security yake ashughulie mwenyewe, wapishi wake ashughulie mwenyewe. Swali langu ni hili kwamba, dunia nzima mtu ambaye anachukua wadhifa kuwa kiongozi wa nchi anapostaafu hupewa hadhi fulani inayostahiki kiongozi wa nchi, na baadhi ya heshima anayopewa ni pamoja na ulinzi wake, security yake, kwamba ukiwa kiongozi wa nchi utakuwa na marafiki wengi, lakini pia utakuwa na enemies wengi maadui wengi. Sasa ukisema security ya Rais, ni sawa na security ya Mkenya yeyote; basi mtu anaweza kusema pia hata akiwa katika mamlaka asipewe securiy yeyote manake ni kama Mkenya mwingine. Sasa sijui msimamo wako ni nini?

Benard Mwaka Wanjila: Mimi ningependa katika katiba mpya tuwalete marais wawe baadhi ya watu sisi wawe one of us,

hii maneno ya mtu kupewa mamlaka mingi hii inaleta hata ndio ina(?) akiwa anajiona kama ni raia anatembea kama na raia na hatakuwa na(?)

Com. Zein Abubakar: Kuna mpango wowote(?) raisi ambaye anakaa hivi.

Benard Mwaka Wanjila: Mimi ninajua raisi huyu wa Eritrea, ambaye anatembea akiwa huru.

Com. Zein Abubakar: Wacha nikuandikishie Isias Arferwoki ambaye ni raisi wa Eritrea sasa anaulinzi vile marais wengine wanaulinzi. Na hata alipokuja Kenya, alikuja na walinzi wake, wacha huko kwao, akija Kenya huja na walinzi wake, lakini ni maoni yako sibishani ngoja kidogo.

Com. Mosonik Arap: Na ulisema kwamba package ya president, iwe kama yawa Kenya wote, sio tu security. Sasa Wakenya wengine wote wana package ya aina gani?

Benard Mwaka Wanjila: Kuna formula ambaye imeandikwa(?) retirement package na other public servants the same formula should apply when it comes to the president.

Com. Mosonik Arap: Can you just enlighten us in which way.

Benard Mwaka Wanjila: For example if a Kenyan who retires receives a monthly pension so that(?) that it can remain 35% of the salary the retiring president should also get the same 35% of(?)

Com. Mosonik Arap: I also have one last one, you said that the tujadiliane kwanza international conventions kupitia bunge, pengine kwa ajili zinaweza kutofautiana na utamaduni wetu. Okay, kuna plan ya conflict between our culture and the international conventions.

Benard Mwaka Wanjila: Kwa mfano kuna sheria hizi zinazohusu watoto, sheria ya kimataifa inazuia wazazi hata saa hii katika mashule, wanasema watoto wasichapwe viboko; na katika mila na desturi zetu, mtoto kuchapwa sio eti anapewa punishment as such, lakini anarekebishwa, ili awe mtoto mzuri na akuwe mtu ambaye anaheshimu watu wengine na sheria.

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo wewe unasema, kukiwa kuna miktaba ya mataifa ambayo nchi yetu inaingi ndani ya miktaba hiyo; kwanza tuwe na njia ya kuipitisha katika nchi yetu na pili ilingane na mila na desturi zetu.

Benard Mwaka Wanjila: Ndio.

Com. Zein Abubakar: Asante sana, uende pale ujiandikishe, utoe hiyo memorandum umeandika. Sema kitu kidogo haraka.

Benard Mwaka Wanjila: Kulingana na hiya maswali naweza kusema kitu kidogo. Sasa naona kwa sababu ya hiyo.....(?) ambayo tunasukuma nayo, kuna sheria nyingi hapa Kenya ambazo zinakuwa adopted na zinapingana na maadili yetu na zina pitishwa sisi wananchi wa Kenya tunaumia tukisikia. Labda bunge imepitisha sheria sasa wanawake wapewe mamlaka zaidi, vitu kama hivyo na sasa tunashindwa na sasa mbona hawatulizi sisi tunasikia tu.....

Interjection Com. Zein Abubakar: Ngoja ndugu yangu, maana mbona hawatulizi sisi maanake nini kuna kura ya maoni.

Benard Mwaka Wanjila: Maanake sisi wananchi kuna mambo mengine hapa kwetu ambayo yako na utaratibu wake lakini wakati tunasikia sheria imekua passed kwa bunge huko ama imetoka.....(?)

Interjection Com. Zein Abubakar: Nipe mfano wa mambo ambayo ungependa wewe kuhusika katika kuyaamua kwa kupigia kura ya maoni kama Mkenya, mambo gani?

Benard Mwaka Wanjila: Sasa wakati inakuwa kama hii sheria ya watoto kutoadhibiwa, ya viboko haya wakisema usawa wa kijinsia, hiyo kitu gender quality. Kuna hii kitu wanasema genital mutilation, hiyo maneno yaani circumcision ya wanawake. Inalingana tena na circumcision ya wanaume. Watu wanatoka Ulaya.....(?)

Interjection Com. Zein Abubakar: Hiyo FGM wacha mimi nikuambie, FGM hailingani na ya wanaume kabisa.

Benard Mwaka Wanjila: Unajua wakianza na FGM wanakuja pia kuinterfear na our method of circumcision. Yaani wanasema FGM ni mbaya.

Com. Zein Abubakar: Wewe unapendekeza wanawake waendele kutahiriwa?

Benard Mwaka Wanjila: Hiyo ni mila sisi hatuwezi kupendekeza hapa, kwa sababu hapa hatutahiri wanawake; na hatuwezi kwenda Ukambani tukasema wanawake hawafai kutahiriwa na sisi hapa si mila yetu. Kwa hivyo hiyo iwachiwe. It's a cultural base tuwachie watu wenyewe kama hapa sisi kwetu wanaume wanatahariwa kwa njia fulani, hata sio wanakuja wanasema hiyo njia mnayotumia si nzuri.

Com. Zein Abubakar: Lakini usiwe na wasiwasi sijasikia mtu yeyote akisema wanaume wasitahiriwe. Asante sana. Au mumesikia kuna mtu amesema hivyo. Asante sana kwa maoni yako, juiandikishe ningependa kutambua kufika kwa Mheshima Angatia karibu Mheshimiwa. Tunaendelea na kuita watu, Alfred Kivuvi Wakuha karibu mzee.

Alfed Kivuvi Makoha: Kwa majina naitwa Alfred Kivuvi Makokha. Ningependa kupendekeza mbele ya tume ya kurekebisha sheria, ya kwanza kuna hapa Kenya unaletea pale mtoto halafu asomeshwe(?) natetea sheria ya wanawake nimejaribu.....(?) na sisi wazee nayo na maoni yangu naona hakuna mtu ambaye amejaribu kutetea wazee ikiwa umezaa watoto na umezeeka nao watalindwa namna gani?

Com. Zein Abubakar: Tunataka mzee utaje na upendekeze maoni yako.

Alfed Kivuvi Makokha: Pendekezo langu ni hili, ningetaka mzee kama amezeeka, kama ana mtoto, na amejaribu kufundisha mtoto, mtoto naye pia amsaidie. Kwa sababu watoto wengine wakienda hawawezi mjali mzazi.

Interjection Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo unataka katiba iwajulishe watoto wasaidie wazazi wao, si usema hivyo na unyamaze.

Alfed Kivuvi Makoha: Eh katiba ilazimishe watoto, watoto hawa wawe wakisaidia wazazi wao.

Pili, katika kuajiriwa kazi naona watu wakiajiriwa kazi(?) wanaajiriwa tu na hivi mtu akitoka huko kama mtoto alikuwa amejiriwa mwalimu, ama askari polisi lazima ana(?) naona viza nyingi sana za uvunjaji wa sheria tuwe na form maalum, mtu akiajiriwa kazi kama ni officer, police officer, army. Awe amejaza form na hiyo form inaonyesha ya kwamba tangu aajiriwe nyumbani hana shamba, nyumbani hajakaa(?) wazazi wake wamekaa maisha.....(?) ya umaskini. Huyo akiajiriwa kama amejaza form kwanza mambo ya kwanza achunguze mshahara yake ni pesa ngapi? Ya pili kama ameo apatiwe.....(?) mahari kama wazazi wake ana nguvu amsaidie kama hana nguvu mwenyewe afanye hivo.

Tatu ndio tumalize hii mambo ya judgement kwa sababu hao wakiajiriwa, eh wanaenda kulima.....(?) wengine wanatoka huko wanaoa wanawake wengi(?). Sasa wakifutwa kazi ndio wanatoka huko(?) na kuharibu amani yetu.

Niko sasa kwa upande wa mwongozi, hapa Kenya tuna rais.....

Interjection Com. Zein Abubakar:(?) hukutambia(inaudible)

Alfed Kivuvi Makoha: Kama hapo tuna president wetu Moi sasa anaenda kureture, akita sijui akiongea neno, ama neno moja kama vile tunaona hapa kwetu ati president akitaka kuwacha atawachia mtu na anamfanyia campaign.....

Interjection Com. Zein Abubakar: Sasa mzee ashatoka hapo nyumbani niende.....na nini. Ngoja tukubaliane, nilisema hutaji jina la mtu, au sikusema hivyo ametoka kwenye au hajatoka kwenye line? Ukitaka kuto mapendekezo sema raisi anayestaafu asifanya hivi na hivi. Sijui kama tenaelewana. Haya.

Alfed Kivuvi Makoha: Raisi aliyestaafu asifanyie campaignie mtu. Awache tu kazi yake na wenyewanasimama wasimame na raia wachague wenyewe.

Kila mkoa ipate nafasi ya kutoa president, ili kila mkoa ipate kutoa mtu.....(?)

Com. Zein Abubakar: Mimi nina swali ndogo sana, uliposema wazee katiba iwalazimishe watoto wao kuwasaidia wazazi. Je wale wazazi wasiokuwa na watoto watasaidiwa na nani?

Alfed Kivuvi Makoha: Wale wazazi wasiokuwa na mtoto serikali iwasaidie.

Com. Zein Abubakar: Asante sana mzee. Bwana Jacob Emshitalo. Naomba radhi kwamba ikiwa sikutaja jina vizuri, mzee utaniambia vile linatamkwa, karibu mzee wangu, karibu mzee.

Jacob Sidialo: Kwa majina mimi ni Jacob M. Sidialo, mimi nina maneno masaba au sita hivi nataka nichangie. Neno la kwanza land matters succession, when aparent passes away the process followed to transfer a land from the deceased to the dependant is very long and expensive. Kwa hivyo tunaonelea mashamba, ikiwa baba amekufa amewacha watoto, tuna wazee wa vijiji ambao wamejua hao watoto. Hawa wazee wa vijiji ndio wanaweza kuangalia mambo ya shamba ambalo baba ameiwacha. Lakini mambo ati uende ushtaki kaburi kortini sijui kwa kaburi sijui kama mtu anaweza kuamuka tena aende afanye ushahidi kwa shamba lake. Kwangu mimi naolea ya kwamba, sheria ya Kenya, yaani mambo ya shamba kushtaki; mtu ambaye amekufa hiyo inachukua pesa nyingi hata watoto wenye kuwachwa ni maskini hawawezi kupata shamba kwa sababu wanakaa tu humo na tena mtu mwingine anaweza kufa na mwingine akufe, sijui unaweza sitaki nani.

The president should be aged above 42 years; a younger person should not be a president.

Interjection Com. Zein Abubakar: Unataka 42 chini(?)

Jacob Sidailo: 42 kuenda mbele. Kuenda juu.

Interjection Com. Zein Abubakar: Akiwa na miaka 100 sawa.

Laughter from the audience

Jacob Sidailo: Mimi naonelea namna hiyo kwa sababu.....

Com. Zein Abubakar: Sawa mzee endelea. Ingingine .

Jacob Sidailo: Nyingine ni, girls should not be given land by the parents, as this will break the institution of marriage and the family. Yaani nasikia tu ati mambo inaanza kupitishwa pitishwa saa ingine eti msichana apate shamba kwa baba yake, tena mvulana apate shamba kwa baba yake. Wasichana wengi watakuja kuharibu nyumba zao kwa sababu wanaonelea ya kwamba hata nikiwacha huyu mwanamume, nitaenda kupata shamba kwa baba yangu. Hiyo naonelea ya kwamba, hiyo sheria ikipitishwa inaweza kuwa nzuri, kwa sababu hapa kwetu kwa vile ninaona kama akina dada akiwa ameolewa mahali na arudi kwa baba yake na akufe, sisi hatuwezi kumshika hapo mbele tunamshika nyuma. Si namna hiyo.

Interjection Com. Zein Abubakar: Ukiona tunaitikia temeelewa na usitafute support kuto kwa watu kule. Useme si ni hivyo halafu watu wanaitikia eeh. Yaani sasa unafikirai hiyo point itakuwa nzito zaidi. Wewe unatoa ushahidi kwa tume, tosha kabisa hiyo mzee.

Jacob Sidailo: Namba mne, every Kenyan should only hold one job. Mimi naona watoto wengi wanateseka hapa wameilimishwa na hakuna kazi, na ukiangalia watu wengine wako na kazi tatu, kazi nne, kazi tano, na hao watoto wamekaa tu namna hii.

Namba tano, every province should have different laws, as we have different culture. So that our culture can apply when making important decisions. Like marriage, care for children.

Treatment of debts, mimi naonelea hii utungaji wa sheria ingeendelea kwa mikoa kwa sababu kila mkoa wako na mambo yao, mambo yao; lakini ikiwa ni pamoja namna hii tunaweza kuchukua mambo ya huko kwenu tunateta huku. Nachukua mambo ya kwetu hapa napeleka huko kwenu.

Interjection Com. Zein Abubakar: Sasa mzee umetupa mfano mmoja ambao unasema sheria iwe na tofauti katika kila mkoa. Mfano wa kwanza umetoa ni kuhusu ndoa, tupe mifano mingine ambayo sheria itakuwa tofauti kulingana na mikoa.

Jacob Sidailo: Nyinge ni kuhusu kutahiri hii. Kuna watu wengine wanatahiriwa na wengine hapana.

Interjection Com. Zein Abubakar: Sawa nyingine.

Jacob Sidailo: Nafika hapo tu.

Com. Zein Abubakar: Yaani sheria hii italingana na mila na desturi za watu wa eneo hilo.

Jacob Sidailo: Eeh.

Com. Zein Abubakar: Lakini point ingine sasa?

Jacob Sidailo: Point ya sita. The president should protect all provinces in the country, give every province a chance to lead the country. Yaani.....

Interjection Com. Zein Abubakar: Mzee si wewe wakwanza tuwe tunasikiza wengine wakisema, he is not the first person to recommend rotational presidency on the basis of provinces. Kwa hivyo ukiwa umekubaliana na yule alitoa mwanzo unasema mimi naunga mkono hiyo, kama unataka tujue tumeelewa. Ni hivyo mzee tumeelewa hii. Unapendekeza kwamba rais atoke kutoka mkoa mmoja baada ya akimaliza kipindi chake yule atakayefuata rais wa kutoka mkoa huu asisimame tena, wa mikoa mwingine ndio asimame, unataka hivyo?

Jacob Sidailo: Rudia tena.

Com. Zein Abubakar: Kwamba katika uchaguzi, akichaguliwa rais kutoka mkoa mmoja kipindi chake kikiisha, ikifika uchaguzi unaofuata wasimame watu wa mikoa mingine, mkoa huo ungojee mpaka izunguke katika mikoa mingine kisha ndio itarudi katika mkoa huo.

Jacob Sidailo: Sindio nataka namna hiyo.

Com. Zein Abubakar: Sawa sawa.

Jacob Sidailo: La saba na ni la mwisho, sisi tuko na watoto, na hao watoto tunawapatia walimu waelemishe hao watoto. Ni mtoto lengo lake akikosa ni kuchapwa viboko, lakini nasikia sasa mambo inaanza kuzungumzwa ati.....

Interjection Com. Zein Abubakar: Mzee hiyo lugha tumesikia, pendekeza tafadhali.

Jacob Sidailo: Nataka mniruhusu nisome tafsari kwa bibilia hapa, mimi ni pastor na niko na *laughter from the audience*. Nataka nisome proverbs mlango wa 23 na mustari wa 12. Inasema hivi, “apply your heart to instruction and your ears to words, knowledge do not withhold correction from a child for if you beat him with a rod he will not die. *Laughter from the audience*.”

Interjection Com. Zein Abubakar: Toa mapendekezo.

Jacob Sidailo: Sasa mimi noanelea ya kwamba, watoto wakichapwa, walimu ni walimu ambao wanaweza kufundisha watoto, na mtoto akikosea akichapwa anaweza kurudi kwa njia. Mimi naonelea ya kwamba ni vibaya sana kupea, huko kwetu tunalima na ng’ombe, upewe dereva ng’ombe kwenda kulima kwa shamba na uchukue misharati sasa hapo sijui hizo ng’ombe zinaweza kulima kweli? Mimi nafika hapo na mchango yangu.

Com. Zein Abubakar: Asante sana mzee kwa kutupa pia mafunzo ya bibilia. Sasa tunamwita Peninah Msungu mwanafunzi, kiasi Peninah anaenda kuitwa, nimwite Milimo Peter, student. Peter Milimo, eeh Sammy Bushasha, kiasi anakuja Peter usitoke nje tena nitakuita pamoja na Peninah nitawaita.

Sammy Bushasha: I am Sammy Bushasha and I would like to say the following. A government officers serving in any capacity once he is involved in fraud or corruption of any nature should be sacked and not be transferred.

Second, agriculture being the backbone of our economy should be tax free by the government this way, no license to import any agricultural product e.g. sugar, milk products and many others. When we can produce the same, the relevant bodies of e.g. sugar board should be the ones to issue such licenses after ascertaining the situation and discovering there is a shortage, or there is a shortage, somewhere, in short we should not import what we can produce ourselves.

This has led to collapse of our industries e.g. KICOMI, sugar companies like Muhoroni and many others. That is what I had.

Com. Zein Abubakar: Asante sana ndugu uende pale ujiandikishe na utuwachie hio memorandum. Sasa narudi kwa mwanafunzi Peninah Msungu. Peninah kama hayuko, ah Milimo Peter, unakumbuka nalivyosema Milimo utaje jina lako shule yako, darasa lako na miaka yako.

Milimo Peter: I am Milimo Peter from Shamoni secondary school, I am in form four East and I am having the collective views from my fellow students.

Interjection Com. Zein Abubakar: How old are you?

Milimo Peter: I am 20 years old. We as students we want free education the for youth from primary level up to University level. This is because we find that, we have some children who come from poor families, and we see they are clever but they don't get education.

We should have people we students after school we want to be assured of jobs, because we find that some of us after school, we start loitering we do things which lead us may be into death, or some other problems.

Then we have seen that corporal punishment should be back to school because we find that prefects have had hard time to correct students who are problem to schools because they know without being caned. So you find that a student after doing a mistake when you take him to a teacher, he knows very well he is not going to be beaten so next time he will just repeat the same mistake. But if a student is punished or beaten, they will know that if I repeat the mistake I will be beaten, so he will not repeat the mistake.

Then we want that each school should at least have a doctor or a nurse, because you find some schools come from outskirts of the lets say we have the Kakamega General Hospital. Your see some schools when students or pupils feel of fall sick they don't get quick first aid, so we would like the government to make sure that each school has a nurse or a doctor.

Then there must be specialization in taking some subjects right from primary schools up to university level. Such as when we have sciences one should just specialize in sciences right from primary up to University level.

Then we should have cost sharing in institutions such as schools or health centres. You see...

Interjection Com. Zein Abubakar:(Inaudible)

Milimo Peter: Yes.

Interjection Com. Zein Abubakar:(Inaudible)

Milimo Peter: You see the government says that they are paying something....

Interjection Com. Zein Abubakar: I am just saying you just proposed that you should have free education, why do you want to have cost sharing again?

Milimo Peter: We want the government.....

Interjection Com. Zein Abubakar: You have the government to share, a cost sharing in health and other matters.

Milimo Peter: So those are what I had.

Com. Zein Abubakar: Okay just hold on, what if you say you want the government to give job assurance to all students.

Milimo Peter: Yes.

Com. Zein Abubakar: What if there are no jobs? What should happen?

Milimo Peter: They should at least give some money, then they give to these who have finished schools they start something small like a business.

Com. Zein Abubakar: Thank you very much go and sign our register and give us the memorandum you have written. Sasa narudi kwa Penina Msungu, has Peninah come? Peninah you remember I said please give, how many copies of that do you have?

Penina Msungu: My name is Peninah Msungu from Shamoni secondary school, I am 19 years old, a form four and these are the points that I am going to talk about constitutional review.

The presidential powers to be trimmed, by this I mean they should be arrested whenever he has done any mistake. For example we find that sometimes the president trying to criticize some leaders or some people because he see that he cannot be arrested. And therefore we are asking the government that not to honor so much the president such that he sees that whenever he does anything wrong he cannot be corrected or he cannot be reacted upon him.

Secondly, schools should be categorized under one class and by this I mean, day schools, boarding, national, provincials, districts and harambee schools should cease, because facilities are not equally distributed or exams should be set according to the levels. Because you find schools like Alliance girls comparing with Shamoni we are having the same syllabus but these people at Alliance have a lot of facilities they learn a lot comparing to us who just get a little bit of education because sometimes we don't have facilities, or we don't have enough teachers.

Another one, countrywide secondary schools should have low fees, by this I mean schools which are in remote areas like Shamoni comparing with schools like Starehe boys, you find that sometimes they are indicating on the newspaper that we should have the same amount of fees being paid and it's very cumbersome sometimes for those parents who are taking their

children in remote areas like some of us. This happens because he or she took this student to this remote school because that is the much he could afford.

Interjection Com. Zein Abubakar: What do you want to be done?

Penina Msungu: We want the fees to be lowered in the school, which are in upcountry.

Interjection Com. Zein Abubakar: So you want the fee structure to vary according to the status of either urban or rural.

Com. Zein Abubakar: Who pays less.

Penina Msungu: The rural schools.

Com. Zein Abubakar: The rural schools okay.

Penina Msungu: There is also lack of confidence in the National Examination Council, because there has been this problem of leakages each. And every year and we are wondering if some of us are struggling very hard to attain at least to get a very good grade at the end and you find some school they are just starting for the main exam while some of us are just trying very hard, we don't know where the exam is set, but we are just trying to visualize where it's coming. And some like may be right know as form fours are preparing for the exams, there are certain school who already have leakages. They are just studying for the main exam.

Interjection Com. Zein Abubakar: Peninah could you name some of these schools for our information. Taja taja taja Peninah. You know I will tell you this, if there are such things going on it's already illegal under the current issue, legal structures it's illegal. And if a school is known to be doing that, they can even be deregistered the whole class of that year can be deregistered. You know that eh. But I am not trying to put you on the sport, if you don't want to answer that go to the next point.

Na katiba isimruhusu raisi kuwa na uwezo wakifalme, kwa mfano wakupendekeza mtu fulani apewe mamlaka fulani kama kiongozi bila idhini ya wanaohusika. Huyu raisi apewe tume ya kuchunguza mienendo yake ili kwamba akivunja sheria apelekwe mahakamani. Na yeyote anayetaka kusimama kwa kiti cha urais ni lazima apitie kwa kiti cha ubunge ajitahidi apite kwa kiti cha ubunge ili achaguliwe pia kwa kiti cha rais na akipoteza cha ubunge atapoteza vyote.

Nakuja kwa urithi, ningependekeza kwamba speaker aongoze nchi akishauriwa na mkuu wa sheria wakati kuna uchaguzi. Matokeo ya uchaguzi wa rais yatangazwe na tume ya uchaguzi kama vile anavyofanywa kwa kiti cha ubunge. Na rais aliyechaguliwa aanze kazi baada ya kuapishwa. Huyu raisi aapishwa na judge mkuu akishauriwa na viongozi wa makanisa.

Mahakama, tunahitaji mahakama inayowatumikia raia wote sawa bila kujali rangi ya mtu, kabila au dini ya mtu. Afisa yeyote wa mahakama akipatikana na makosa ya ufisadi apewe adhabu kali pamoja na kupoteza kazi yake. Nafasi ya kuajiriwa kwa mahakimu na majudge kuwe wazi kwa mtu yeyote aliyehitimu kama mwana sheria bila kuchunguza dini yake, kwa sababu sheria itamtumikia sawa watu wote.

Na mahakama ya kidini iondolewe kwani sheria itamhudumia, itahudumia sawa watu wote bila kujali dini ya mtu. Hiyo sheria pia inajulikana inalinda haki ya mwananchi bila kudhulumu, au kulazimishwa na kuhangaishwa na mtu yeyote.

Uhuru wa kuabudu, thehebu lolote lililosajiliwa kisheria, isiingilie taratibu za thehebu lingine bila yakukubaliwa na thehebu linalohusika, wala kulilazimisha kufuata taratibu saa zote zilizo za mafundisho ya dini hiyo. Kwa mfano tukiwa na sherehe ya mathehebu mengine kama Wakristo, kuna lazima ya kwamba hawawezi kutengeneza au kuchinja ng'ombe yao bila idhini ya Waislamu, wala kuku ama kondoo hauwezi kuchinjwa kufanywa kitoweo kwa sherehe hizo., Waislamu watawalazimu washtakiwe, la sivyo Muislamu atachinja na kufanya taxation ya kazi yote na hii ni kazi nyingine au, ni imani nyingine isiyo ya dini hiyo.

Vyombo vinavyotumika kwa kazi hiyo na Muislamu ni sawa na vyombo ambavyo thehebu lingine linavyotumia na hatutaki mambo kama hayo kuingilia makanisa mengine. Kusiwe na raia, kusiwe na sheria inayoruhusu makanisa mengine. Kusiwe na raia, kusiwe na sheria inayoruhusu dini yeyote ile kulazimika kutumikia dini nyingine kimabavu na kuharibu imani ya hao kiroho.

Upande wa mashamba: Mambo ya title deed ipunguzwe na iwe kama shilingi mia moja kwa sababu mhusika huwa ametoa maarifa mengine kwa survey na hata kwa land control board kuidhinisha shamba hilo kwa mwenyewe. Wizara kama ya

physical planning hatuoni kazi gani inafanya kwa mashamba ya watu; ili kuiboost malipo au hand out kwa kazi hiyo yao. Inafaa hizo handouts ziondolewe.

Nakuja kwa usawa: Tunapofikiria, kuhusu jambo hili la usawa, tufikirie pia mipaka iliowekwa na Mwenyezi Mungu, kwa maana anayeoa ni kama muajiri na anayeolewa ni msaidizi ambaye hawezi kuwa na mamlaka ya kuongoza huyo aliyemuoa.

Kwa hivyo jambo la usawa, liwe tu katika watu wenyewe walioona kusikizana.

Health insurance: Ningependekeza kwamba, kila raia apewe nafasi ya kuandikishwa kama alipiwe health insurance na serikali, jinsi serikali inavyofanya taxation ya kila kitu raia anachonunua. Nafikiri yangu yamefika hapo. Ni asante sana.

Com. Mosonik Arap Korir: Subiri kidogo, asante. Utapendekeza kwamba mgobeaji wa kiti cha Rais, awe na uwezo wa kifedha na kijamii, hatukuelewa hiyo ulimaanisha nini.

Mathayo Mashinde: Kwa sababu, bwana commissioner, mtu akiwa hana fedha huenda akahangaika na kukopakopa kwa watu, na huyo hatakuwa na sifa za kuwa kiongozi. Na mtu ikiwa hana uwezo wa kijamii yaani vile anavyoishi, personality yake na mambo mengine hatakuwa na uwezo wa kuamua yale yanayotakikana kwa taifa lake.

Com. Mosonik Arap Korir: Lakini hujanijibu, uwezo wa kifedha awe na shilingi mia moja ama million moja, ama ni nini?

Com. Zein Abubakar: Swali linaloambatana na hilo mzee, yani kwa lugha ingine, watu wanaogombea uchaguzi wawe matajiri peke yake. *Noises from the crowd* Hiyo ni maoni yake, tunataka ufafanuzi ndio tunayoandika tujue, lakini msimwingilie, hayo ni maoni yake. Sema mzee usiogope, sema vile unavyotaka.

Mathayo Mashinde: Mtu ambaye anayetaka kugombea kiti cha urais, inatakiwa awe na shilingi million mia moja kwendelea mbele; kwa sababu mtu atadaiwa madeni kwa kukopa na huenda akapoteza mali ambayo ni ya family, ambayo haikusimama kwa jambo hilo.

Com. Zein Abubakar: Asante sana mzee, uende pale ujiandikishe kama umetoa maoni kwa tume ya kurekebisha Katiba. Sasa nina, wewe nani? Josphat who? Josphat Patidi, ngoja, ngoja, ngoja tufuate sheria, nilimuita mara ngapi huyu? Ulipokuwako, nilikuita? Ulikuwa hapa? Kwa nini hukuitikia? Kama ulikuwa huko nje, kwa nini useme uongo ndugu? Sasa ngoja, ngoja, kama wewe tulikuita ulikuwa hauko, nenda pale kwa programme officer, utoe jina lako, atalinganisha na orodha yetu, atatupa sisi ushauri. Enda uzungumze na programme officer. Sio unakuja ati unakaa unajipa wewe mamlaka ya kusema. Tafadhali nenda pale kwa programme officer, umpe jina lako halafu atatushauri. Sasa kuna dada ambaye alikuwa anasema hakuja kutoa maoni lakini amebadilisha anataka kutoa maoni Mary Shimweni. Karibu dada.

Mary Shimweni: Tume ya uchaguzi, mimi kwa majina naitwa Mary Shimweni, nina jambo moja tu ambayo ningependa nitoe maoni yangu. Commission ya kurekebisha Katiba nina jambo moja tu ambayo ningependa nitoe oni juu lake na ninaangalia katika as we strive to create a just society in Kenya kuna areas ambao hatuangalii, hawa watoto ambao wanaitwa street children, mara nyingi watakuwa watu wazima na hawana belongings, sasa wanaona kama ni watu ambao wanaweza kutenda chochote. Ninapendekeza ya kwamba, serikali itafute njia ya kupatia hawa watoto maybe wajenge centres ambao hawa watoto wataita kwetu, ili tupunguze hawa watoto katika streets za urban areas in Kenya. Kwa sababu wakiendelea hao ndio watakua tatizo kwa hii nchi yetu. Napendekeza ya kwamba watafutiwe mahali hata kama ni adoption, au ni nini, lakini wapate mahali pa kukaaa. Nashukuru kwa sababu ni shatoa maoni yangu mahali pengine, lakini hili ni pendekezo ambalo nilisahau kwa ajili ya muda na nimeona nilitoe hapa. Asanteni.

Com. Zein Abubakar: Asante sana dada Mary, lakini unahitajika pia ujiandikishe pale leo. Nilikuwa nimeitengea nafasi hii Joshua Pakisi, endelea.

Joshua Patisi: Majina yangu ni Joshua Patisi, nina vipengere kumi na mbili, kipepengere cha kwanza napendekeza tuwe na serikali ya umoja wa kitaifa.

Kipengele cha pili Rais akichaguliwa asiwe Mbunge kusema ya kwamba anawakilisha eneo fulani fulani. Kwa ajili tunajua cheo

cha Rais ni jukumu kubwa akiakilisha eneo fulani fulani itakuwa kazi nyingi kwake. Napendekeza ya kwamba sehemu hiyo ingeliwachiwa mtu mwingine. Napendekeza ya kwamba bunge ipewe mamlaka jinsi ya kuongoza mambo yake yenyewe, jinsi ya kujua muda ambayo itakuwa katika kazini, na muda ambao itadumu na tena itaisha ili iwe na uhuru wa kuendesha mambo yake. Isiwe chini ya Rais kusema kwamba bunge hili nalivuja kwa muda fulani,

Interjection

Com. Mosonik Arap Korir: Excuse me. The chairmans permission, you made your views, you started very well the first one when you just finished it and it was very direct, government of national unity, president not to be an MP, Parliament to have its own caledar, just do it like that.

Joshua Patisi: Thank you, thank you, asante Kipengele cha nne, kuhusu kazi, twajua ya kwamba nchi inayokua lazima iajiri watu wake, na hili limekuwa tatizo la nchi hii, Napendekeza kazi kupewa wale ambao wanaohusu kutoka vyuo mbalibali.

Kipengele cha tano ni kuhusu corruption, napendekeza ya kwamba, Katiba hii ipewe anticorruption moment nguvu, ili iwe inachunguza hayo mambo.

Kipengele cha sita, napendekeza government resources ziwe zinagawanywa sawa sawa katika kila eneo, tuseme maji, moto, yaani electricity.

Kipengele cha saba napendekeza elimu ya nchi hii iwe elimu ambayo inakuwa na mpango, yaani imekuwa stable, ili tusiwe na kusema kwamba serikali inayokuja inaingiza elimu hii, ingine inakuja inabadilisha, sasa imefanya elimu ya nchi hii haijakuwa na mizizi yake.

Kipengele cha nane, napendekeza wabunge wasiwe na mamlaka kusema kwamba tumejiongezea mshahara shilingi fulani, Mshahara uangaliwe kulingana na budget. Tuseme ya kwamba hiyo yote iwe inakatiziwa, na yule ambaye anasimamia mambo ya fedha.

Tisa, napendekeza tuwe na ugawanyaji wa resources za national resources kwa usawa.

Jambo lingine, napendekeza tuwe na kupeana madawa kwa wagonjwa wa ukimwi na wawe wanachukuliwa kama wananchi wengine. Napendekeza, tunaunga mkono wale ambao waliotaja ya kwamba tuwe na matibabu ya bure, kwa ajili wananchi wa nchi hii ndio wanawachangia kwa kutoa kodi na mambo mbali mbali. Asante.

Com. Zein Abubakar: Asante sana, uende pale ujiandikishe na maandishe utupe. Namuita sasa Ezekiel Mukabana, halafu ndio nitamuita Josphat Lucheli Nyamu. Wewe ni Josphat, baada ya mzee Mkabana uje hapa.

Ezekiel Mukabana: Mimi yangu nitasoma tu kwa sababu iliandikwa na washiriki wa kanisa. Mimi ni pastor Ezekiel Mukabana wa African Church of the Holy Spirit Box 183 Shinyeri ya Kakamega, ilioanzishwa mwaka wa 1927.

Interjection

Com. Musonik Arap Korir: When mzee came here, he told us it was registered in 1952, is it the same church?

Ezekiel Mukabana: Katiba, ilianzishwa mwaka wa 1927

Interjection

Com. Musonik Arap Korir: Excuse me, African Church of the Holy Spirit, of the Holy?

Ezekiel Mukabana: Spirit. Yes.

Com. Musonik Arap Korir: That's a different one, sorry, you know we want accurate records, nilisikia mzee akisema, 1952 sasa unasema 1927, are they branches of the same church or the same church?

Ezekiel Mukabana: That's what I thought. Sasa hili unasema mtu kwa registrar, kwa certificate.

Com. Musonik Arap Korir: I remember mzee was saying, when we have

Interjection

Ezekiel Mukabana: Labda ni hotel.

Com. Musonik Arap Korir: Ngoja Bwana, now I'm getting rude because you don't want to listen to me. We just want to clarify. Unasikia? Mzee alipoanza, akasema tukiwa tumesema nani ni kiongozi wa kanisa, watu wengine wasiingilie makodi, si ni kweli? Sasa umetaja ile ile kanisa, na umetueleza ni mwaka wa ishirini na saba, na mzee alikuwa amesema hamsini na mbili, can we have it clear?

Ezekiel Mukabana: Sasa, ile ambayo ninazungumza, yangu ndio iko clear, iko kwa registrar, ndio kwa certificate, labda huyo aliwapoteza, unajua kuzungumza na hata unaweza zungumza ya hapa au upoteze mwaka. Watu wanasema pesa sio kwa nguvu, labda alisahau.

interjection

Com. Musonik Arap Korir: No, I'm not arguing with you Bwana, because I'm not the registrar of societies. Now is that a different group? Unajua mzee alikuwa anasema kwa niaba ya kanisa vile nilielewa, sasa is it the same church exactly, or you have another cogregation or something?

Ezekiel Mukabana: Labda tucalculate kwa miaka lakini ni kanisa moja.

Com. Zein Abubakar: Kulingana na record niliandika, mzee Musa chimose, alizungumzia siku ile iliteuliwa kiongozi, wewe unazungumzia siku chache ilikuwa registered,

Ezekiel Mukabana: Hey, Hey, kiongozi

Interjection

Com. Zein Abubakar: Hebu mzee tufafanulie tu, isiwe kazi ndefu, useme tu mara moja mzee.

Ezekiel Mukabana: Ishirini na saba ndio roho mtakatifu alichagua watu kutengana, hao wanaenda Nairobi, na hawa

walibakia _____ katika Kaimosi cells, halafu

Interjection

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo mzee unasema haya ni makanisa mawili tofauti?

Ezekiel Mukabana: Ee, sasa, sasa, hii, huyu maneno yetu ni moja isipokuwa sheria yetu ilitengwa 1952 na mtu ambaye alikuwa anatengeneza Katiba alikuwa _____ na mtu wakati alipata register ya kanisa hilo.

Com. Zein Abubakar: Sawa, basi keti tushasikia mzee. Keti hapo, wewe utoe maoni yako.

Ezekiel Mukabana: Haya, mimi naota kama okay, inaenda hivi, sisi wafuazi wa African Church of the Holy Spirit, tunahuzunika ama tunahangaika sana na mambo ya kort, kort na serikali, na kanisa pia inaongea mambo ya serikali. Wakati kunapopatikana mzozo kati ya viongozi wa kanisa, na wamepelekana mahakamani kutatua nani atakayekuwa kiongozi, badala ya mahakama kuamua ya kuwa waumini warudi nyumbani wale wamchague kiongozi ambae anaweza kuwalinda, mahakama inapendelea na inaamua tu fulani ndiye anaweza kuwa kiongozi. Hio tunaomba serikali ijayo iwaachie makanisa kuamua ni nani atawalinda. Hata kama hana mali lakini ana roho ya Mungu ambaye anaweza kuongoza watu, anaweza kulinda.

Mambo ya wamama na wazee ama mume na mke. Kanisa limeonelea ya kwamba, mtu wa kwanza alikuwa Adam, akafuatiwa na Eva, hiyo inamaanisha ya kwamba mume ndio kichwa ya nyumba. Na ikiwa sheria zingine zinasema ya kwamba mama awe na nguvu kwa nyumba, watu wawili, wakiwa wote na nguvu, hawawezi kuishi, kwa sababu mama haki yake aliambiwa ya kwamba atazaliwe na atawacha familia yake na ataenda kwa jamii ingine kutengeneza huko nyumba yake. Kwa hivyo, kanisa linasema hivi, mama awe chini ya mzee, kufuatana na mamlaka, kazi anaweza kufanya tu, kama ni kuandikwa anaweza andikwa. Na kuna wengine ambao hawafanyi kazi na wanaishi tu nyumbani wanafanya kazi ya kutengeneza nyumba, watoto, na kubadilisha hiyo tena ni kazi sio tu wamama wapewe mamlaka ati hata wawe President. Mwanamke akuwe president? Hata ukizaa mapacha, kuna yule wa kwanza kutoka, ndiye mkubwa, na bibilia inakwambia ya kwamba kutoka kitabu ya mwanzo, ishirini na nne, inasema ya kwamba Adam ndiye wa kwanza, kwa hivyo heshima sana mkifanya mama na baba wawe sawa, dunia itapasuka.

Inaudible interjection

Ezekiel Mkabana: Ya, nilikuwa nafanya break tu. Mambo ingine, ni mambo ya viwaja ya kanisa na ya shule, kuna makanisa na shule, hata shule, serikali imetuma huko walimu, hata bendera ya serikali, na hizo plot hazina number lakini kuna headmaster, kuna bendera inapepea huko, lakini kufanya juu na chini waone ya kwamba hiyo iko registered imepewa number, hakuna. Kwa hivyo naomba hivi, serikali ijayo, ikiwa inawezekana, itengeneze mambo ya viwaja ya shule na ya makanisa, kwa sababu makanisa na serikali ni kitu kimoja. Muwapunguze tena mambo ya _____

Mambo ya kuridhi mashamba, hiyo nitafanyia tu correction kidogo ama nitaongezea zangu tu kidogo. Baba yako amekuachia shamba ya acreru tatu ama nne, na amewacha watoto karibu saba. Sasa mukienda mambo ya kuridhi hiyo shamba, wanamwambia shiringi ile ambayo imeshida hata hiyo shamba kununua gharama.

Inaudible interjection

Ezekiel Mkabana: _____ okay sababu zimekuwa _____ unajua bado mtu ana maoni yake. Hata ukileta hapa chakula huyu aweza kula pia na huyu akule kidogo, huyu anaingilia, lakini bado ufike mahali wana haki.

Com. Zein Abubakar: Unataka ikifika dakika tano nikwambie zimeisha dakika tano? Maanake ziko karibu kuisha,

Ezekiel Mkabana: Karibu namaliza tu. Kwa hivyo nataka(?)

Interjection

Com. Zein Abubakar: Eh, sasa ulikuwa unasema utasoma, sasa unasoma halafu unawacha kusoma, unarudi tena nyuma unazungumzia yale ambayo ushazungumzia.

Ezekiel Mkabana: Kuna pahali nimeachililia, vile nilikuwa nimeandika.

Com. Zein Abubakar: Eh.

Ezekiel Mkabana: Ya.

Com. Zein Abubakar: Usijirudie lakini tafadhali.

Ezekiel Mkabana: Okay, karibu namaliza tu, kwa hivyo mambo ya mashule na kuna mambo ingine ambayo ni administration, utawala kuanzia assistant chief, chief, DO, kwanza DO, wakisikia ya kwamba kuna pastor ama mhubiri fulani, wamesikia tu fununu, ati anafanya kitu fulani, hawa wanamuambia tu bila huyo kiongozi ninaweza kumwendea kwa njia gani. Wanamaibisha mbele ya watu, mbele ya watoto, sasa ukifika kwa police, ikifika kesho hakuna makosa ambayo ulifanya, wanakurudisha nyumbani. Sasa nataka warekebisha namna hii, serikali ijayo ikiwa inaweza kutusaidia, ikiwa mhubiri ama kiongozi wa kanisa amefanya kosa kidogo, wamuendee pole pole, kwa njia inayositahili bila kumaibisha mbele ya watu. Ni hayo tu, yangu imekwisha.

Com. Zein Abubakar: Asante sana. Hiyo memorandum, hiyo utatupatia tusome, ulisema utasoma lakini umeamua kusema kutoka moyoni, utoe hiyo memorandum halafu saa ile unajiandikisha, ile point aliraise commissioner, you make sure that we are clear the difference between church ile ya mzee na church yako.

Ezekiel Mkabana: Hata sasa hii ninaweza kweli kuleta Katiba?

Com. Zein Abubakar: Hapana, sikiza mzee wangu, mimi sibishani na wewe kuhusu Katiba. Nasema, kama kuna tofauti ya makanisa hayo,

Interjection:

Ezekiel Mkabana: Sio tofauti.

Com. Zein Abubakar: Haya, nenda kajiandikishe, basi.

Ezekiel Mkabana: Aliyetangulia ndie alipotea kidogo.

Com. Zein Abubakar: Kaandikishe basi. Haya, Josphat, utaje jina na uendelee.

Josphat Nyamu: Majina ni Josphat Cheli Nyamu from Shomoni, Box 44 _____ yangu ni kuhusu mavasi. Inajulikana wazi kutoka nyuma hapa Kenya mavasi ya wanawake inajulikana ni marinda, vile kila mtu anajua, na ya wanaume pia inajulikana. Lakini imekuja hivi karibuni, wanawake wameita mfano wa nchi ingine, wanavaa long,

Interjection

Com. Zein Abubakar: Josphat, unajua sasa ukianza kunihaidithia hivyo, hatutajua tuweke nini kwenye Katiba, wewe pendekeza, unataka je?

Josphat Nyamu: Mimi ninaomba mtengeneze sheria ile itaondoa, itapinga wanawake wasivae long, kwa hivyo hiyo inawaibisha ama maubile yao haiwaruhusu. Mengi wamesema, ni hiyo tu nilikuwa nimembaki nayo.

Com. Zein Abubakar: Asante sana Bwana Josphat. Hakuna swali, tafadhali ujiandikishe pale kwamba umetoa maoni kwenye tume ya kurekebisha Katiba. Asante sana. Nafikiri wale wanaoanza kupiga kelele huko nyuma, walikuja wamechelewa, hawajui mzee. Ni yule yule mzee wangu anayefanya fujo, mzee? Mzee? Hebu ngoja, ngoja mzee, hebu niangalie mzee, mzee niangalie, unaitwa je wewe? Jina lako? Taja jina lako, nataka utaje jina nisikie, Jina lako?

Christopher Iad: Unisemee?

Com. Zein Abubakar: aaa, taja jina mzee.

Christopher Iad: Unisemee?

Com. Zein Abubakar: Mimi mzee ndio chairman wa hii kikao, naomba unitajie jina lako. Ngoja mzee, wewe ndio

Christopher? Nasema na wewe mzee.

Christopher Iadi: Christopher ____

Com. Zein Abubakar: Basi ngoja mzee nikupe mwelekeo, utaje jina, uanze kutoa maoni.

Christopher Iadi: Mimi naitwa Christopher Iadi, mimi ni mzee wa tatu, mini sikusoma, lakini pendekezo yangu iko namna hii.

Nimependekeza kwanza Rais Moi, nilienda nikamuapisha mwaka 78,

Interjection:

Com. Zein Abubakar: Mzee, mzee, nilisema tusitaje majina,

Christopher Iadi: Christopher Iadi, kitu mimi nataka kupendekeza kwa nyinyi ni hivi, ni uzazi. Unaweza kuwa umezaa watoto wasichana na unasomesha hao watoto, na hao watoto wanakuja kuzaa watoto wengine na wanakuwachia hao watoto. Tunataka mpatie miaka ya mtu akizaa kwa mtoto yako, mtoto, ikiwa miaka sita ine, akuje achukue aende na mtoto yake. Kwa sababu sisi wazazi tumefika hapo, na muweke gharama ya mtu huyu kulipa mzazi.

Neno la pili ni hawa police. Police wanakuja usiku kama saa kumi na mbili kuingia kwa boma yako, hata wewe hutengenezi pombe, hata yule anatengeneza pombe wanamshika, kama mimi nina wanawake watatu, wawili, anaingia nyumba hii, anapata mwanamke huyu, wana shika na pombe kwetu, anawacha yule mwenye pombe, anakuja kushika mwingine. Anapata hata huyu amekaranga kuku yake ama nyama, anakula, hii nini? Nimeona watu wa Malava, police ya Malava.

Com. Zein Abubakar: Sasa unataka je?

Christopher: Nataka hawa watu wapolic wapewe mamlaka ya kushika mtu. Akiwa nayo wa mshike, akikosa nayo wasimshike na kumkulia pesa yake halafu wanashika na wanamkata pesa bila kortini. Wanachukua pesa yake elfu mbili elfu moja. Hao police wananyanya raia.

Com. Zein Abubakar: Wasijipe mamlaka ya mahakama?

Christopher: Ya. Neno ya tatu, sisi tukitahirisha watoto ama msichana wako akienda harusi, tunatengeneza pombe ya busaa. Sasa pombe ya busaa mnakuja mnajengewa watu wanakaa wanakaa mnajadiliana, Ugo, yaani mahari. Sasa mahari kutakuwa ng'ombe kumi na mbili, ama kumi na tatu, ama nini, na mnakunywa hiyo pombe. Sasa mnasikilizana mnafanya agreement na mnakunywa vinywaji ya pombe ya busaa. Hapana chang'aa, hatutaki chang'aa lakini busaa. Nataka busaa wakubaliwa watu wa busaa wazee wa zamani wakunywe busaa. Wasijaribu kukimbizwa mara kwa mara.

Neno lingine, tunataka maneno ya vile mtu alisema ardhi, maneno ya shamba, wapunguze gharama ya uridhi, kwa sababu mtu anaweza kuwa na watu kumi, wanaume unajua wa hapa wanazaa watoto hata ishirini, na sasa akitaka kushtaki _____, anaona ni pesa mingi sana, wapunguze hapo.

Neno lingine sasa hapo, upande wa katiba. Kama tumesema hapa katiba, msigeuze Katiba ya Shamoni mpeleke huko Nandi, mpeleke wapi, msem maneno ile sisi tulisema hapa na iende kwa bunge. Mimi Christopher Iadi

Intejction

Com. Zein Abubakar: Asante sana Mzee Christopher, uende pale ujadikishe, lakini kwa vile nimekuheshimu, nikakupa fursa uzungumze kabla ya watu wengine kwa sababu ulikuwa una hamu ya kuzungumza, sasa usingilie watu wengine. Jiadikishe basi mzee, asante sana Mzee, asante. Haya kwa vile nimempa mzee mbele, sasa nirudi tena kwa list, Emily Angatia. Mama karibu.

Emily Angatia: Tume ya kurekebisha katiba ni asante, namshukuru. Sasa langu la kwanza napendekeza kulikuwa na loan za watoto wote, niseme wanafunzi kutokea 1974 kwendelea. Hakukuwa na kusema ati huyu ni watajiri na huyu ni mtu masikini. Napendekeza loans zipewe wanafunzi wote wanaenda university, iwe private au iwe ya serikali.

Ingingine, naunga mkono mama yule alisema ati mtu akifiwa, akiwacha mme au akiwacha mke asiridhi kwa sababu ya HIV. Mtu ajitenge tu, asimame kama mme, kama mke, na ajisimamie. Napendekeza, sijui tutafanya nini na mambo ya ukimwi. Serikali

ingechunguza ijue vile tulikuwa na maradhi ya kukoma, halafu watu wote wana ukimwi. Nafikiri tunaweza punguza, serikali itufanyie hivyo. Wawekwe pamoja, watibiwe, wakiwa wamepoa sasa tutakuwa na mambo mzuri, wajengewe mahali wakae pale, sana sana watoto hao wanawachwa. Kama wako na ukimwi, kama wako na HIV, wapewe mahali pakukaa halafu nafikiri Mungu akipenda tutapunguza haya magonjwa.

Neno lingine ni napendekeza mke na mme wakiwa na mke wasikilizane na mambo ya kudhuru mwingine kimapenzi, kiafya, serikali ichunguze hayo. La mwisho napendekeza shule za kutokea chini kwenda mbele na watoto wale tunakaa wasichana, nimeshangaa kusikia ati mtoto wa miezi tisa, amewachiwa baba na baba amemuji nafisi sasa raping a child of that kind. Is it human? Sasa ninataka ikiwezekana serikali iweke sheria ya kuguard hawa watoto na wakina mama, wasichana especially.

Com. Zein Abubakar: Achukuliwe hatua gani?

Emily Angatia: Hata maisha iende nayo, wamumalize tu kwa sababu akirudi ataendelea kunyanyasa wengine.

Com. Zein Abubakar: Asante sana mama.

Emily Angatia: Mm yangu ni hayo. Asante.

Com. Zein Abubakar: Asante sana mama, uende pale ujiandikishe kwamba umetoa maoni kwenye tume.

Emily Angatia: Mungu amubariki.

Com. Zein Abubakar: Asante sana, hata wewe mama asante. Lazarus H. Wasia,

Lazarus H. Wasia: Macommissioners, jina langu naitwa Lazarus Hada Wasia kutoka West Kabras, hapo Lukume na nimeandika memorandum na nina maneno mawili tu matatu ya kupendekeza. Yangu nataka kuongea juu ya parliament.

Parliament imepatiwa mamlaka kubwa kushinda kiwango na kwangu ningependa kupendekeza ya kwamba tungerudisha senate. Senate kama ingerudi halafu mambo ikipitishwa kwa parliament, ije ipoeshe. Hapo kwa senate, tulikuwa tumechagua kila mwaakilishi kutoka kwa kila district anakaa kwa senate. Wawe wakiongea maneno ikitoka huko kama vile walipitisha pesa yao ya mshahara bila kujulisha hata wananchi. Inaweza kuwa hapo na ipoeshe hapa halafu tujue itakuwa namna gani.

Neno lingine linahusu mambo ya mashamba, watu wameongea zaidi lakini ya ukweli iko ya kwamba serikali ilichukuwa hiyo shamba. Hakuna cha kusema kupunguza pesa ya mambo ya kuridhi, serikali _____.

Nina neno lingine ambalo sijui serikali iko namna gani. Maconstitution mumepatia watu ya advocates, auctioneers doctors. Powers nyingi hata charges sijui serikali kama inaweza rekebisha hapo, mwananchi wa kawaida ajue ya kwamba akienda kwa daktari ni kiasi gani ya pesa inatakiwa kwa gani na gani. Kwa maana ukienda kwa daktari, unajikuta ya kwamba unalipa pesa ambayo hata huwezi kujua utafanya namna gani. Hata hiyo pesa, hata ukipatiwa shidano sijui si moja au ngapi unaambiwa tu ulipe shilingi elfu ngapi, na kua shida sana kwa wananchi.

Auctioneers naye akija pengine una deni, achukue ng'ombe mbili, ng'ombe tatu. Wakati wewe unaenda huko kwa deni ya shilingi elfu kumi, elfu tatu, unakuta hata anakudai tena pesa ingine na ameziuza ng'ombe na mwananchi wa kawaida hajui ni sheria gani hawa watu auctioneers wamepatiwa. Ningependelea ya kwamba serikali ichukue hatua, ione ya kwamba watu ya auctioneers wananchi wamekuwa protected na sheria. Na vile tumesema vile advocate, unakuta tu kesi iko anakwambia pay so much money, hata hujui hiyo kesi ni ya aina gani.

Muongezee hapo, nataka kuongea mambo ya mayor. Mayor kweli amechaguliwa na hawa watu, lakini ile kazi anafanya inakuwa ya watu kama for example Kakamega Municipal, kunakua na mayor na huyu mayor anataka afanyie municipal council.

Na vile amechaguliwa na coucncillors na hata nashidwa area gani anaweza fanya kazi nzuri nielezane nayo. Ningependelea achaguliwe na hawa wa municipal hao wamupigie kura kwa maana yeye anachaguliwa kwa hiyo municipal ama county council apigiwe na hao watu.

Com. Zein Abubakar: Apigiwe na macouncillors, au na municipal yote, na wafanyi kazi wake?

Lazarus H. Wasia: Anatoka kwa area, halafu anaingia anakuwa councillor, halafu councillors wanampigia kura ya umayor.

Lakini mimi napendekeza kwamba apigiwe kura na watu wa municipal.

Com. Zein Abubakar: Inaudible question.

Lazarus H. Wasia: Hapana, iko memorandum lakini haina, naongezea tu. Halafu, this political parties, foreigners wanafanya tunagongana. Tunataka first pesa yao itoke kwa sisi members kuliko foreigners kuleta pesa kwa chama hii, kwa chama hii, halafu wanagonganisha wananchi kwa njia ambayo haifai hata kidogo. Na ninapendekeza ziwe vyama tatu. Yangu imekwisha.

Com. Zein Abubakar: Halafu utoe hiyo memorandum, asante sana mzee. Sasa nitaita majina ya watu wengine tuone tunapokwenda. Joseph Alukware, Si nilikuwa nimekuita? Basi joo ukae, wacha niite wengine wajue vile wanafuatana. Philip Muarati. Uko, Rosemary Sikasi, nini mum? Sasa ngoja nikwambie mama, ngoja, ngoja mama, ukiona nimemuita mtu akae, ni vizuri umuache, either uinue mkono nikutambue, sio uje umutoe halafu ukae. Lakini kwa vile umekaa, sitaji jina lako tena, mara ya pili halafu utuambie.

Speaker: Asante, nilikuwa tu kuweka.

Com. Zein Abubakar: Aaah, uanze na jina mama. Kaa utaje jina lako tena, halafu useme kile umesema umesahau.

Angatia: Mimi ni Angatia. Nilisahau, bunge isiwe mchezo. Watu wameenda huko, tumewachagua, wameanza kupigana huko, sisi wananchi tunashangaa, ni watoto au ni watu wamekomaa? Sheria iweke kulinda bunge. Asante.

Com. Zein Abubakar: Asante mama, asante sana. Nimekuita Bwana. Pole kwa ... urudi ukae, keti halafu usubiri. Philip umesema upo? Rosemary Shikasi, uko. Isaiah Muheri, Alfred Watai, halafu Jonathan Werunga. Jonathan Warunga? Timothy

Makale, Cyprian Lumumba. Uko? Daniel Kisukia. Nicholas Shem. Hezron Makunda. Sasa, hao ndio watu watakaofuatana na kulingana na register yetu, hakuna mwingine amejandikisha kwamba anataka kusema. Au yupo? Ulikuwa umejiandikisha mzee? *End of side A*

Na ameenda kuangalia memorandum anarudi. Lakini si swali ile uliuliza mimi, mimi nimeuliza, nilikuwa nauliza swali lingine, ngoja niite wengine. Jonathan Makhoha, Laban Wafula. Nasema yani, mzee wangu sijui kama utanielewa vizuri. Nasema, kulingana na register zetu, hao ndio watu wa mwisho kujiandikisha. Kuna mtu mwingine yeyote ambaye alikuwa anataka kusema na hakisikia jina lake? Yuko? Hakuna mtu mwingine? Haya, sawa. Twende na mzee Joseph Alukwe. Utaje jina mzee wangu halafu uendele.

Joseph Alukwe: Mimi naitwa Joseph Alukwe Juma naye natoka Sieboto, South Kabras, na swali yangu inasema katika Kenya tumeona mtu anayeitwa masikini anashida tena hatabuliwi namna gani. Sheria ya huyu masikini kusaidiwa sijui iko wapi, nyinyi ndio mnaweza kuniambia.

Com. Zein Abubakar: Ukiniuliza mimi maswali leo, haitatusaidia sisi, ngoja, ngoja, nyinyi msinipigie kelele tafadhali. Mzee jaribu utwambie, hao masikini watasaidiwa vipi?

Joseph Alukwe: Iko hivyo, ni asante zile zenye kunyorosha kwa sababu nikuzungumza. Masikini mara nyingi ukienda kwa kila idara ana shida kufanikiwa ile kitu anataka. Hiyo ndio neno langu la kwanza na ningeomba msamaha kwa sababu nilikuwa na memorandum na nilisahau mnakuja hapa leo sababu nilisitushwa kwa njia wamekuja halafu nikakosa kuchukua hiyo. Hiyo ndio neno ya kwanza na nilitaka masikini asaidiwe kwa sababu ni mwanadamu. Mungu anajua tajiri, mwenye kusoma na masikini ni mtu moja tu, ni mtu. Masikini akumbukwe.

Na neno ingine kufuatana na hiyo neno la masikini ambao hapo zamani tulikuwa na watu wakisoma na sisi hatukujua watu walikuwa wanatoa wapi pesa, serikali ilikuwa inafanya ile kitu tunaita loan yenyewe ina gharamia kwa njia ya kitambo kidogo lakini vile tulipata uhuru ilibakia kwa shule inayoitwa university. Ndio ilikuwa ikisaidia sasa tena ina watu. Sasa watoto wa shule wenye kusoma ni wachache sana. Wanaweza kusaidiwa na njia gani?

Com. Zein Abubakar: Sasa ngoja mzee. Kwanza umesema unataka masikini apate huduma katika idara za serikali bila kubaguliwa, hiyo nimeandika. Sasa unasema habari ya elimu na loan, unataka elimu iwe vipi?

Joseph Alukwe: Elimu ichukuliwe na serikali.

Com. Zein Abubakar: Iwe bure?

Joseph Alukwe: Ya,

Com. Zein Abubakar: Sema hivo basi kwenye microphone. Unajua ukisema nataka umasikini, elimu iwe hivi, huduma ya afya iwe hivi, mambo mengine yawe hivi, hiyo ndio tunaandika tu.

Joseph Alukwe: Huduma ya shule iwe kwa serikali.

Huduma ya hospitali: Huduma ya hospitali mnakubaliana na mtu wakati unavyolipa pesa, mtu huyo apone, halafu unapata mtu huyo amepona, halafu unapata mtu huyo amekufa. Na ndio wanakubaliana zaidi. Sasa nikakosa kujua serikali inaweza kusaidia wamasikini kwa njia gani? Kwa sababu ningechukua hiyo nafasi namna vile ninavyosema kwa shule, hospitali na hata nikiunga mkono vile walivyoelezea wandugu na wadada, hata kwa mashamba ya kutoa kodi. Hiyo nafikiri nimemaliza hapo, ninaenda kwa neno la mwisho.

Neno la mwisho, ufisadi, hii mambo ya ufisadi ni neno ambayo ni kubwa, na hata ni neno lingine ambalo huwezi kueleza ukamaliza. Ufisadi watu wanaweza kuwa hata mkoa mzima na mtu mfiisadi ni mmoja. Amechukua mali ya mkoa, na huyu mtu akishikwa pengine atapelekwa jela, ati anahojiwa, hii mambo ambayo wameweka sheria hukumu mtu mfiisadi, haitoshi kitu. Inatakiwa hata itolewe.

Com. Zein Abubakar: Auawe?

Joseph Alukwe: Ee,

Com. Zein Abubakar: Unataka mtu akishikwa na hiyo kosa la ufisadi afanywe vipi?

Joseph Alukwe: Yeye na ukoo wake utoke.

Com. Zein Abubakar: Maana ya kutoka maanake nini?

Joseph Alukwe: Maana ya kutoka, hii mali alikula ni ya mkoa mzima ambao ni watu hawawezi kuhesabika. Kwa hivyo hata ukimshika umueke hapa, hiyo mali bado inamkinga tu, atolewe na ukoo wake, ndio mali irudi kwa watu hao.

Com. Zein Abubakar: Aaa hujanielewa mzee wangu, unasema maanake ni nini? Ahamishwe, au unasema kutolewa ni kuuawa?

Joseph Alukwe: Apigwe risasi.

Com. Zein Abubakar: Yeye na ukoo wake?

Laughter

Joseph Alukwe: Yee.

Com. Zein Abubakar: Sawa, tumesikia, asante sana. Hayo ni maoni yake msimwingilie. Na umesema ndio ya mwisho hiyo.

Joseph Alukwe: Ndio ya mwisho.

Com. Zein Abubakar: Asante sana mzee wangu uende pale ujiandikishe.

Joseph Alukwe: Nilikuwa nimeandika.

Com. Zein Abubakar: Ee, lakini pale unajiandikisha kusema umetoa maoni. Philip Mwarati,

Philip Mwarati: My names are Philip Maina Mwarati. I have some proposals on the following:

Presidential powers: currently the president has alot of powers given to his office. I propose that most of the powers, like choosing judges, the high court, court of appeal, those powers be reduced.

Com. Zein Abubakar: You say reduce the power of appointing judges maanake nini?

Philip Mwarati. The President currently is the one who appoints judges of the high court, he also appoints judges of the court of appeal.

Com. Zein Abubakar: Yes, unataka je?

Philip Mwarati: I only propose that they get us a different body to be appointing judges of this particular body.

Secondly, the stage of qualifications, currently we have just, he must be a Kenyan, over 35 years, he must be holder, I want to propose that a president, on the qualifications he must be a degree holder. This is because we want people who can interpret policies and formulate policies to the country.

Also a law must be formulated to bar the president from making presidential appointments especially in private and public sectors. This is when somebody goes for someone who goes for president, you will hear Wamalwa, Wafula, in all the public sectors and what have you.

Interjection

Com. Zein Abubakar: Who should appoint the public officers?

Philip Mwarati: We have the Public Service Commission but it is overridden by the president. The chief's act was recently reviewed and removed. I want to propose that we must have a law because currently, we have criminals who do a lot of criminal activities may be at night but because wananchi don't have a way of arresting and accusing then because lack of evidence, they go free. They go posing during the day because formerly the chief was empowered if you could suspect anybody, while arrest and detaining for any suspicion of criminal activities. Currently criminals are operating free because there is no law unless you take him and arrest him with exhibits. So law should be formulated that can protect people of a given area, if they know this person is a kind of _____ or a robber and causes of evidence that can allow members to be detained, so that the public can be free and secure.

Com. Zein Abubakar: So you want the chief to be given the powers to detain people without evidence?

Philip Mwarati: When I was saying formerly it was there, and it used to help but it was abused. but if it can be re-introduced in a formal way it can also help.

On unemployment, currently all graduates from most universities or colleges are not employed. I propose that the government give this people loans without security to enable them start their own business or whatever so that they can live like any others who are educated.

On matters affecting the security of the state and any other foreign policies, I want to concur with these people who gave the views earlier that we must have opinion polls. Opinion polls on anything that affects the security of the state, to know what Kenyans are saying about research because somebody says Kenyans are saying this and he has not consulted the Kenyans themselves. So we must have a opinion polls, that can empower somebody to talk on behalf Kenyans.

Com. Mosonik Arap Korir: Opinion polls or referendum? Because opinion polls somebody can take a sample from you people, say Kenyans wamesema hivi and they are just surveying may be 10,000 people and saying these are representatives for

Kenyans. So would you want conducted opinion polls conducted by newspapers or like a referendum?

Philip Mwarati: Well, even referendum can do then I have no problem.

Tunafanya njiani ndio tupate mkebe ya chakula, ili watoto wapate chakula. Na sasa wakienda shuleni watoto wanafukuzwa juu ya pesa ya mjengo; na huko shambani muwa iko, na hiyo muwa kupata permit ni shida dhidi mpaka utoboke shilingi elfu mbili, ama elfu tano ndio upate permit. Sasa hiyo ndio shida yangu hapa risafu na watoto wanasoma sina, la kufanya sina kazi yeyote.

Mimi nafanya boda boda barabarani. Ni bahati sana kupata hata shilingi sitini. Nikija kutegatega tu serikali yetu ikipenda inaweza kutuonea huruma hapo kuhusu shule, na kuhusu upande wa ukulima.

Shamba ni yako mwenyewe, muwa ni yako mwenyenye lakini kupata tu permit ya kuingiza miwa ndani ya factory, mpaka utoboke; na huko watoto wanataka chakula, huko watoto wanataka uniform, sasa hapo tumeshindwa tuko wapi? Tunaenda wapi? Yangu ni hayo tu.

Com. Zein Abubakar: Asante sana ujiandikishe upande ule, nenda ujiandikishe pale. Nicholas Shem, mbona unainua mikono kijana, kijana sema. Sijaita jina umeinua mkono. Nicholas Shem, baada ya Nicholas Shem ni Hezron Makunda akae karibu, sawa.

Nicholas Shem: Asante sana commissioner mimi sina mengi nemesikia wameongea ile nilikuwa nimepanga lakini nataka kuongezea tu. Naongezea hivi; kuna shida upande wa mahakama kuna mzee alisema kuhusiana na mawakili. Mzee wakawaida anakuwa na shida kuendeleza kesi yake, kwa sababu gharama imekuwa kubwa. Kama kungukuwa na mpango fulani tupate body ambayo inaweza kusaidia wananchi wakawaida. Tuseme kama vile tuko na hii chama ya wanawake wa FIDA. Kama tunaweza kuwa na ingine ya kusimamia hiyo, kusaidia mzee wakawaida akiwa na kesi yake.

Pili, mzee wakawaida amekuja kortini; waakili anamvuruta huyo mzee akili mpaka mzee anashindwa atasema nini. Kwa mfano mzee amekuja kwa kesi yake la shamba halafu amefika hapo; wakili badala ya kumuliza mambo ya shamba, anamuliza wewe

mzee uko na wanawake wangapi? Sasa zile mzee anaulizwa hivyo akikata kujibu akisema mimi nimekuja juu ya mambo la shamba, magistrate anamwambie jibu swali. Sasa inabidi huyo mzee aseme ako na bibi watatu; halafu amechanganya alikuwa amekuja kwa maneno ya shamba.....

Interjection Com. Zein Abubakar: Sasa unataka je?

Nicholas Shem: Inatakikana kuwe na mpangilio, kama umeenda kwa kesi ya shamba unaulizwa mambo kuhusikana na shamba. Na kama labda umeulizwa na wakili, magistrate naye awe na uwezo ya kumwambia wakili, aulize maswali kulingana na vile wamepeleka makaratasi yao kortini.

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo wewe unataka njia zinazotumika mahakamani ziwe rahisi na zinafahamika vizuri.

Nicholas Shem: Yah, ndio mzee wa kawaida apate kuelewa, amekuja kwa kitu fulani. Ijapokuwa shida nyingine ni kwamba tumeanza kuona hata ukiwa na haki, umejaribu keuleza mambo yako, mtu wa kawaida mwenye amekaa huko anaona kweli umesema mambo ya maana. Hii ni kwa sababu kumekuwa na corruption, unakuta ile yote ulisema ya maana inatupiliwa kesi yako imetupwa. Sasa hii corruption, hata tumeanza kufikiria maybe in future lawyers watakosa kazi. Kwa sababu lawyer anaenda kurepresent mzee, anasema haki za mzee, halafu lawyer mwingine naye anajaribu njia zake, vile anavyoweza kukutana na magistrate na nini na nini, sasa huyu lawyer anapoteza hiyo kesi sio ati hakupresent inavyotakikana. Lakini kwa sababu ya corruption. Sasa tumeanza in future may be mawakili atakosa kazi kama magistrate

Interjection Com. Zein Abubakar: Sidhani wewe utalia sana mawakili wakikosa kazi, nafikiri unataka ufisadi uondolewe katika mahakama.

Nicholas Shem: Ndio hiyo, ndio hiyo. Halafu kitu ingine ya mwisho ni upande wa wafanyi kazi wa serikali. Unapata wewe mzee ama kijana, umeenda kwa ofisi ya serikali kusaidiwa, vile unavyo chukuliwa unanza kutetemeka, unaona kama umeenda mahali penye hauna uhuru. Kwa mfano umeenda kwa ofisi fulani unataka kitu fulani wanakuambia enda hapo uandikiwe, ukisha enda hapo kuandikiwa umekuja na karatasi mtu anakuuliza, wapi jina lako. Na wewe wakati uliambiwa uende pale hukuambiwa utaenda uandikiwe jina na nini unambiwa tu enda hapo upewe karatasi. Inatakikana kuwe na njia ya kuelimisha watu ambao hawajui, ndio mambo yote ikuwe rahisi kwa watu, wazee wakawaida ama akina mama wakawaida. Ni hayo nilikuwa nayo mengi wamesema.

Com. Zein Abubakar: Asante sana, uende pale ujiandikishe kwamba umetoa maoni kwa tume ya kurekebisha katiba. Mtu wa mwisho katika horodha ya majina yetu ni Hezron Makunda.

Hezron Makunda: Asante sana, kwa majina najulikana kama Hezron Makunda, kutoka Maira South Kabras. Jambo la

kwanza mimi napendekeza, katika nchi hii tuwe na matibabu ya bure kwa kila mwananchi; kwa vile hivi sasa matibabu imekuwa gharama ya juu, na wananchi wa kawaida wengi wanashindwa kugharamia. Ugonjwa unaweza kushika mtu wakati wowote, na kama hana pesa anashindwa kujitibu. Kwa hivyo tuwe na matibabu ya bure.

Jambo la pili, napendekeza kwa upande wa elimu, serikali iwe na mpango wakuhakikisha watoto mayatima, ama wale watoto wamezaliwa kwa jamaa ambaye hajiwezi, wanasaidiwa kuendelea ki elimu. Sasa unapata mtoto amefanya vizuri shuleni, baada ya kufaulu anashindwe kuendelea na masomo ya upili, kwa vile pengine anatoka jamaa maskini, ama hana wazazi na siku hizi hakuna mtu anamshughulikia unaona mtoto anarandaranda tu bile kujua afanye nini. Napendekeza serekali iwe na elimu ya bure kwa watoto.

Jambo la tatu ni kuhusu employment yaani kuajiriwa, tunavyojua watu wengi hawana kazi hapa nchini.....

Interjection Com. Zein Abubakar: Kenya asiyejua kwamba kuna ukosefu wa kazi.

Hezron Makunda: Karibu kila mtu anajua.

Interjection Com. Zein Abubakar: Eh, sasa nipendekezee mambo ambayo tutatumia kudeal na hiyo ukosefu ya kazi, kwa katiba lakini.

Hezron Makunda: Napendekeza kwamba katika katiba ijayo, serikali ilioko mamlakani ipange kujenga viwanda, unajua katika kila sehemu kuna pengine muwa, kuna mimea fulani inakuzwa sehemu ingine, viwanda ijengwe ili ipatie vijana kazi, hiyo ndio pendekezo langu.

Com. Zein Abubakar: Ikiwa bado hakuna kazi, wale ambao hawana kazi watafanyweje?

Hezron Makunda: Yaani hiyo ndio njia moja yakusaidia tupate nafasi za kazi. Jambo la nne kuna wakati mwanamke anaolewa na bwana unapata wanaishi vizuri. Lakini wakati inafika tuseme kibahati mbaya bwana anakufa sasa bibi amebaki na watoto, utapata wale mashemeji wataingilia wanasema sasa huyu hana haki pengine kwa shamba na marehemu bwanake ama watoto hawana haki. Kwa hivyo ningependekeza tuwe na sheria, bibi na watoto ndio watakuwa waridhi wa ile mali ya yule aliaga.

Jambo la tano ni kuhusu matumizi ya pesa ambazo hukusanywa kutoka kwa local government. Mimi naona local government inakusanya pesa nyingi lakini kwa vile hii pesa inaenda in central government huwa ikienda huko hairudi kusaidia wananchi. Tungependa iwe decentralized ili pesa ile inakusanywa Kakamega inafika hapa Kakamega itoke hapo irudi isaidie watu mashambani, pengine kujenga barabara, kujenga shule na mambo kama hayo.

Jambo la sita, jukumu la kufundisha vijana hasa maadili kuhusiana na jamii, yaani family life. Naonelea kama Wakenya wengi wameachia hiyo jukumu kwa walimu na unajua.....

Interjection Com. Zein Abubakar: Unataka aje?

Hezron Makunda: Mimi nataka kuna ile sehemu ambayo inahitajika ifanywe na wazazi kama kufundisha watoto jinsi ya vile wanahitajika wakea wasiwe wanatembea kwa njia mbaya, ili mtoto hata anapata mimba kama hajaolewa, kwa vile amekosa kufundishwa.

Jambo la saba, kuna appointments ambazo nafikiria wale wako mamlakani, wana appoint mtu mmoja unasikia yeye ni chairman wa hii.....

Interjection Com. Zein Abubakar:(Inaudible)

Hezron Makunda: Tunataka mtu mmoja kazi moja ile ya appointed.....

Interjection Com. Zein Abubakar:(Inaudible)

Hezron Makunda: Halafu mwisho napendekeza kwamba ile mamlaka wa rais ipinguzwe.....

Interjection Com. Zein Abubakar:(Inaudible)

Hezron Makunda: Yaani rais anakuwa na mamlaka zaidi...

Interjection Com. Zein Abubakar:(Inaudible)

Hezron Makunda: Kwa mfano kuna wakati unapata rais anaweza kuamrisha kitu fulani kifanyike; kwa mfano, na pengine hicho sio sawa kwa wananchi. Lakini kwa vile yeye ako na hiyo mamlaka amepewa na sheria; sasa inabidi ifanyike, hata pengine kama wananchi wengi hawapendelei. Ni hayo tu.

Com. Zein Abubakar: Asante sana ndugu uende pale, hayo maandishi utuwachie tutayatumia, uandike pale jina lako. Sasa nimepewa list ingine na kama kuna mtu alikuwa anaitwa na anakata kuja ata sema kwa nini anakataa kuja na alikuwa hapa. Jotham Makhoha, nilikuwa nisha mwita tena Jotham, na ameenda ameandikisha tena, na hayuko tena. Jotham Makhoha,

Laban Wafula, kaa hapa. Na Laban ulikuwa hapa toka mwanzo, okay keti. Robert Natiri. Emanuel Kupora songea karibu, Patrick Omwerema songea karibu. John Kariuki. Kwa hivyo nataka hawa watatu waje hapa mbele. Je kuna Mkenya yeyote ambaye alikuwa anataka kutoa maoni yake na hakupata fursa ya kutoa maoni yake? Nitarudia mara ya pili, na kikao hiki kiwe shahidi kwamba narudia mara ya pili. Kuna Mkenya yeyote ambaye alikuwa anataka kutoa maoni yake na hakupata fursa ya kutoa maoni? Basi itakuwa hivyo hao watatu ndio watakuwa wa mwisho kutumalizia kikao kwa vile hakuna mtu mwingine ambaye alikuwa anataka kutoa maoni. Na nyinyi mliondoka mmeshududia hivyo au hamkushuhudia hivyo? Sawa.

Wafula Laban: Yes thank you my names are Wafula Laban. I wish to propose as follows:-

1. That we should have an executive President whose qualification should be a graduate, and the president should be chosen outside parliament.
2. The winning party should have the President; the cabinet ministers should also be vetted from without parliament.
3. And they should be vetted by Parliament, who also should be scrutinize if there are people of integrity, and have the necessary experience for whatever ministry they are to undertake.
4. For a president to be elected, he should have the simple majority of 25% in five provinces, and also 50% of the active votes.
5. I propose that we should have two chambers to put checks in the house, on the Parliament activities like salary; and should anything happen contrary to the two houses, a common system will be able to petition.
6. No persons should be allowed to hold public office in case of any past misappropriation of office procedures or any scandals.
7. The Electoral Commission should be an independent body, and this should be able to be recalled back in case of non-performance. I don't know how you will do it, but you know there you can create your way.
8. A limit of land of 20 acres to every individual, 20 acres of arable land.
9. Harambees should be stopped and a special tax funds to be introduced to minimize corruption.
10. Land ownership should be to all, irrespective of sex, the acquisition of title deed processes should be shortened.
11. Political parties should be limited to a certain number. I cannot suggest the number, but let the rules that are going to be set should be through to minimize only political parties which have what we call national representation.
12. Court procedures should be(?) and they should ensure that there's fairness in their verdicts.
13. MPs or presidents working on voter expectation should be treated as a form of corruption; you see what the voter expects is different from what the official role is, so anybody who is bound to pent on voter expectation should be(?) should be treated as corruption.
14. Any bill or motion that is passed and at any other stage it is found to be defective, the Attorney General should be brought to task.

Com. Zein Abubakar: Asante sana uende ujiandikishe pale na utuwachie hayo maandishi tafadhali, asante. Anayefuatia, taja jina na uendelee.

Emmanuel Par: Kwa majina naitwa Emmanuel Par. Ningependekeza ya kwamba wafanyi kazi wa serikali, and top civil servants and parastatal chiefs; should be vetted by parliament before their appointment, and their duties should be terminated after they have been scrutinized by parliament.

Political parties should be maximized to four in the country, to avoid unnecessary political groupings. Working conditions for civil servants or public servants as a whole, should be set by parliament and should be reviewed after every ten years.

Another one is, the anti corruption unit should scrutinize the expenditure of every ministry or public institutions at the end of each financial year.

Another one, farmers should be given the mandate by the constitution to be in charge of co-operative bodies dealing with farming.

Another one, the government should be empowered by the constitution to set prices for all cash crops in the country. That is all, thank you very much.

Com. Zein Abubakar: Asante sana hakuna swali uende pale ujiandikishe. Patrick Omwarema, Patrick ndio atakuwa mtu wa kuzungumza wa mwisho leo kutufungia kikao hiki.

Patrick Omwerema: Kwa majina naitwa Patrick Omwerema kutoka Mwera sub location na mimi niko na swali walisema mwana Kenya yeyote awe na

Interjection Com. Zein Abubakar: Patrick kwanza leo ilikuwa sisi kuuliza maswali halafu pili, hata swali ulilokuwa ukitaka kutuliza hulikumbuki. Unakumbuka swali ulikuwa ukitaka kutuliza?

Patrick Omwerema: Nakumbuka.

Interjection Com. Zein Abubakar: Haya utulize bas.

Patrick Omwerema: Mwanakenya awe na haki yake, mimi nataka kuliza *end of side A* nikitaka kwenda mahali popote nitafanya namna gani?

Ni kama, jambo la pili wana boda boda wowote wanaweza pata haki yao, wanaweza pata loan kama ni wana Kenya?

La tatu, mimi nauliza, pendekezo kama kuna viwanda hapa tuko na viwanda, lakini lazima utoe hongo hiyo hongo tutatoa wapi ndio(?) hiyo tulipe..

Interjection Com. Zein Abubakar: Yaani unamanisha ukitaka kuajirawa kwenye kiwanda unatakiwa utoe hongo kwanza?

Patrick Omwerema: Sio hivyo.

Com. Zein Abubakar: Eh, ni vipi?

Patrick Omwerema: Kenya yote, kwa maana hata ukitoka hapa ukienda wapi hadi hongo kidogo na sisi tunafanya kwa barabara. Kupeleka tu mtu ndio upate shilingi tano au kumi, hiyo tano uweke shilingi moja ndio utoboke pengine hadi utajiri wanafanya kazi mmoja unaambiwa ati we hufanyi vizuri. Lakini hukusoma utafanya namna gani na watu wenye hawakusoma watafanya namna gani ndio waajiriwe.

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo Patrick unataka wale watu wanafanya kazi ya boda boda wasiulizwe kutoa hongo na wala wasisumbuliwe.

Patrick Omwerema: Eh.

Com. Zein Abubakar: Haya.

Patrick Omwerema: Kuna ingine.

Com. Zein Abubakar: Sema sema bwana.

Patrick Omwerema: Mimi ninauliza nilisikia hapa ati wasichana hata wasipo oleka wapewe ardhi, ni kama hawata oleka watahika ardhi. Ardhi ikuwe yao.

Interjection Com. Zein Abubakar: Hivyi ndio ulisikia Patrick, sasa wewe maoni yako ni nini, unakubali hivyo au unapinga au unasema namna gani?

Patrick Omwerema: Sikubali.

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo wewe hutaki mwanamke awe na haki ya kuridhi shamba, hutaki kabisa hivyo. Hutaki mwanamke ashike shamba?

Patrick Omwerema: Sawa sawa.

Com. Zein Abubakar: Sawa ya mwisho?

Patrick Omwerema: Ya mwisho iko hivi, narudia tu ile nimesema.

Com. Zein Abubakar: Unasikia Patrick ikiwa huna ingine, mimi nimekupa fursa ikiwa una ingine, kama hauna ingine, useme tu yameisha.

Patrick Omwerema: Ingingine nina sema.

Com. Zein Abubakar: Lakini usirudie.

Patrick Omwerema: Kwa nini mimi sikusoma, lakini nasikia watu wengine wanapatiwa msaada lakini mimi niko kwetu huko, ati msaada imepewa mahali fulani, lakini mimi sipati na mimi ni mwana Kenya.

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo anataka msaada ikitolewa isitolewe kwa kubaguana.

Patrick Omwerema: Kwa kila mtu yeyote.

Com. Zein Abubakar: Sawa.

Patrick Omwerema: Asante.

Com. Zein Abubakar: Asante sana Patrick uende pale ujiandikishe kwamba umetoa maoni kwa tume ya kurekebisha katiba. Sasa tumekifunga kikao hiki na ningependa kutambua kwamba kikao hiki tunakifunga rasmi. Lakini kabla ya kumaliza, ningependa kusema mambo mawili matatu, ya kwamba leo kwa vile ni kikao cha mwisho nitampa fursa pia commissioner mwenzangu aseme machache, kwa sababu huo ndio tunafunga kazi kwa mara ya mwisho kabisa.

Kwanza ningependa kushukuru sana wananchi wote waliojitokeza kwa wingi leo kuja kutoa maoni yao na kuhakikishia kwamba maoni yoa tatajimuishwa na yale maoni mengine ambayo tumeyapokea kutoka kwa Wakenya wengine. Patrick sasa

uwe kimia kidogo ili turekebishe katiba yetu. Baada ya kupokea maoni haya, tutakwenda tuyashughulikie na yale maoni mengine tukae chini tuandike report ya kila sehemu ya uakilishaji bungeni. Tunatakiwa kwanza tuandike repoti ya constituencies yaani ya sehemu ya uakilishaji bungeni, tukimaliza hiyo tuandike repoti ya kitaifa ambayo itakuwa inajumuisha na kujulisha maoni ya Wakenya katika sehemu zote hizo, 210 halagu tutoe mapendekezo yaani draft proposal ya constitution au bill. Msuada tuwe tumeutoa. Halafu tutahitajika kuyarudisha mambo hayo kwenu, ili muwe na fursa ya kuchunguza kwamba yale mliotuambia ndio yale tuliyoyaandika, na kwamba mapendekezo yetu yakikatiba yanaafikiana na mambo mliotuambia.

Tutahitajika pia kawa na vikao vya kimkoa, baada ya kuwapa fursa yakuchunguza ripoti zetu ili muje mtupe maoni zaidi kuhusu ile ripoti na msuada ule halafu, ndio tuite mkutano wakitaifa ambao utajimuisha kwa wakilishi wenu wa bunge pamoja na wakilishi watatu kutoka kila wilaya pamoja na wakilishi wa makundi mbali mbali ya kidini, ya wanawake ya wafanyikazi na kadhalika; ambao kwa makadirio itakuwa karibu watu 600.

Katika mkutano huo wataangalia ule msuada tuliyopendekeza, na ikiwa kuna maafikiano ya theluthi mbili; basi msuada ule utapelekwa bungeni. Lakini ikiwa hakutakuwa na maafikiano kuhusu mambo yaliyomo katika mapendekezo yetu ya msuada ya kikatiba, tutahitajika kufanya kura ya maoni katika nchi, ili wananchi wajiamuliwe wawe ndio watu wa kuamua mambo ya mwisho, halafu baada ya hapo turudi tena bungeni. Halafu bunge lipitishie tuwe na katiba mpya. Hayo ndio mambo ambayo baado hatujayafikia leo tumekamilisha hatua moja tunangoje tufikie hizo hatua zingine.

Na pia ningependa kuwashukuru kwa niaba yenu, Wakenya wote kwa sababu nyinyi mmepeata

fursa wa kuwa watu wa mwisho katika kutoa maoni. Wakenya waliojitokeza kutoa maoni yao mbalimbali, na kwamba tunawashukuru watu waliohusiana na sisi katika kufanya kazi hii kuwa kazi nzuri. Tunashukuru watu wa provincial administration ambao kwa mapana ma marefu wamesaidia sana kufanya kazi hii ikawa imefikia mahali ilipo sasa. Tunashukuru sana wale wanakamati wa 3Cs ambao walifanya kazi kubwa sana katika kila sehemu ya uakilishaji bungeni. Twashukuru macordinators wetu kama mnavyojua katika kila district tuna coordinator nchi nzimana hapa ni Caleb Amaswache yeye ndio amekuwa akisimamia kazi ya hapa. Tuwashukuru pia wabunge ambao walikuwa ni wanakamati na watu wote walioweza kutufanyia sisi kazi hii ikawa rahisi.

Na katika sehemu mbali mbali za jamhuri yetu tukufu, tumeweza kupewa ukarimu na kuweza kupewa mahali pa kufanyia kazi, na taasisi mbali mbali. Na kama leo kama tuko hapa tunamshuru sana Principal, kwa kuweza kutupa fursa hii kuwa hapa. Na hili jambo la kihistoria litakuwa katika Historia. Litakuwa katika historia yetu kwamba shule hii ilichangia kufanya kazi yetu ikafana, na kwa miaba yune ningependa kuwashukuru wafanye kazi wa tume ambao wamekuwa wakifanya kazi kwa wengine wenu hamjuu lakini tumekuwa wanafanya kazi usiku na mchana. Ukifika

usiku kuna huko national secretariat yetu kuna wanafanya kazi wanaendelea na kazi asubuhi wengine wanaendelea na kazi usiku.

Ningependa kumpa fursa hii ndugu yangu, na kumshukuru sana tumefanya kazi naye vizuri. Tumezunguka mkoa huu wa Western pamoja, na tumefanya kazi vizuri ningemuomba naye aseme machache halafu ndio atufungie mkutano huu rasmi. Dr. Mosonik Arap Korir.

Com. Mosonik Arap Korir: Yes commissioner mwenzangu Abubakar, Zein Abubakar, na wafanyikazi wenzetu wa kutoka tume ya kurekebisha katiba, bwana Hassan Mohammed program officer, Joyce Wamucii assistant, na Marion Nekesa yule ameketi; sisi tumekuwa hapa leo Malava constituency kikao cha pili kwa ajili lazima kulikuwa na kikao kingine mahali pengine. Tumefanikiwa kwamba kikao cha mwisho kabisa cha tume, kikao rasmi tumemaliza kwenu. Mlielezwa asubuhi kwamba sisi tumegawanywa kwa vikundi vinane na ndivyo hivyo hivyo tulifanya

Kazi. Leo wenzetu walikuwa Emuhaya, Hamisi, Budalang'i, Emuhaya tena yaani Emuhaya ya kwanza ilikuwa Kimwa mission, ya pili Ebungwe, halafu Khwisero, Ekalamane, Matungu. Tumefanya kazi namna hii tangu mwanzo wa mwezi wa tatu 27th of March I think is when we Started tulianza tuliita pilot survey tukafanya majaribio kuona kwamba je kazi hii itawezekana na tuifanye kwa njia gani. Kwanza tulikuwa tumependekeza ama wananchi walikuwa wamependekeza, na nitaeleza ilikua nini, kwamba tuwe na mkutano zaidi ya miwili kwa kila constituency. Halafu tena kukawa na

pingamizi ama problem of time, halafu tukafikiria ama tufanye siku moja ama kikao kimoja mahali. Tukaanzia area ya Nairobi and its environments kufanya pilot survey, tukawa na hakika kwamba kikao kimoja hakitisho kwa constituency; ndio tukaongeza iwe vikao viwili. Kwa hivyo ilikuwa ni mwanzo wa mwezi wa tatu lakini hii ya vikao viwili tulianza tarehe 17 mwezi wa nne. Na tukaanzia vile mwenzangu chairman waleo alieleza, kufuatia serufi wa alphabet. Tulikuwa tunafikiria tuanze wapi, na kama kutahiriwa ing'awa kila mtu anataka lakini hakuna mtu anataka kutangulia awe mbele afikishia wacha kwanza wengine wafanye kwanza ndio tuwafuate tusikie iko nanma gani. Sasa kulikuwa na mabishano tuanze wapi mpaka tukakubaliana kwamba alpha-bet hakuna mti alipanga, tufuate alphabet tu vile iko, ndio tulianza Central province, tukaenda Coast province, tukarudi this way Eastern province, tukaja Nairobi province halafu North Eastern Province halafu Nyanza province, halafu Rift Valley, halafu mukawa wa nyuma.

Na wengine tukasikia kwamba watu walikuwa wamelalamika pengine area hii na Rift Valley kwa ajili gani, sisi wawe wa mwisho. Lakini kama wakati mwingine wanasema wale wa mwisho watakuwa wakwanza, the last shall be the first. Kwa kumaanisha kwamba kwa bahati hiyo alphabet watu wa Western province wakapata muda mwingi kushinda mikoa ile yote mingine ya kujutayarisha, kwa ajili hii nikama mtihani. Mtihani ya kutoa ile maoni na kuhakikisha kwamba maoni imeingia kwa katiba mpya. Sasa nyinyi mlipata fursa ya kujitayarisha mkawa wa mwisho. Na vile tumeona na mwenzangu hapa commissioner. Watu wa Western kila mahali tumeenda they are very organized. Wanaweza kuwa na

maoni tofauti kabisa wanatofautiana, kama tuseme mlima wa Elgon na chini hapa upande huu. Lakini vile wale wanasema na hata hao wanasema wamepanga vizuri. Hiyo nikusema kwanza kwa ajili walikuwa na muda ya kujitayarisha, na tena hiyo ni kumaanisha kwamba wale walikuwa wanafanya kazi kamati the 3Cs the district coordinators, with their MPs and then the providers walifanya kazi nzuri. Kama kazi imefanywa vizuri namna hiyo inarahisisha kazi yetu sisi, kwa ajili tunatakiwa kufahamu vizuri. Na sasa kuanzia hivi karibuni kama vile mwenzangu amesema tutaketi sasa na kwanza kusoma kila mmoja, hii ni folder ya Western province kila province na yake.

Sasa tuanze kuanzia number one, mpaka mwisho nakusema wananchi je walisema namna gani tulipokuwa Kwale, Mandera, walipokuwa Webuye na Malava. Halafu kutafuta sasa the common friends, ikiwa mmepanga vizuri vila mlifanya inatusaidia. Hatukwenda tu kwa constituencies ama kwa mikoa. Kwanza mwanzo mwanzo kama mnakumbuka mwaka jana tulipoanza hii kazi mwezi wa June na mwezi wa July tulizunguka kwanza every provincial headquarters, to launch the process halafu baadaye tukaenda tuliita provincial hearings, tulikuja tena sasa sio kuluanch lakini kusikiza maoni kwa provincial headquarters ndio tukaja Kakamega nakadhalika.

Na tena hiyo kufanya provincial hearings wakati uli ulikuwa wa tukaita organized groups. Ambao tuliwahesabu kwamba hawahitaji civic education sana kwa ajili wamejifunza tayari. Nikifupisha niseme kwamba sasa tunajukumu ya kwenda kusoma, kuelewa na kuandika. Sisi kama tume tulikuwa tumeomba bunge, na tunafurahi mheshimiwa wa zamani yuko hapa. Kwamba watupee muda ya kutosha ndio tusichezee haya mawaidha, hayo maoni ya wananchi. Tukasema mpaka mwesi wa May watu wengi hawakutufahamu wakafikiria pengine tunapenda tu kukaa hivi. Lakini kukaa nikuketi vile tumeketi leo, kila siku tangu mwezi watatu tuko mahali tunaketi. Lakini tunataraji kwamba wananchi na viongozi, wajumbe wa bunge watatuelewa na kutupatia nafasi ya kuandika vizuri. Kwanza kuelewa kwa kusoma na kuandika ndio tutoe ile katiba inayohitajika.

La mwisho ni kusema kwamba, mimi ninafunza Historia University, na nikifikia hivi kwa damu yangu nina elewa kwamba tunafanya historia. Historia tunaifanya making history because ni mara ya kwanza sisi wananchi wote kuketi na kujadiliana kuhusu katiba yetu. Una jua ile ya Lancaster ilikuwa ya viongozi wetu wakisiasa, walienda ng'ambo London. Baadaye wabunge wamefanya kazi nzuri wakarekebisha Katiba, lakini walifanya kama wakilishi wetu bungeni. Sasa hii ni mara ya kwanza tumehuziha wote. And we are proud and happy that we have associated with the process. We want to say may this process bring about the national consensus that we all need. Na tulisema hata vile inafanywa inasaidia, the process and the method is important as the result, kwa ajili watu wataona kwamba it is a result of consultation of working together on the same process.

Sorry Mr. Chairman that I had the opportunity to do that, kwa ajili kawaida, any way I am feeling a bit sentimental so asanteni sana. Let me give him back the microphone, asante.

Com. Zein Abubakar: Sasa ningependa kumpa co-coordinator, pengine coordinator atampa tu fursa baada ya kusema machache, principal atufungie kikao kwa kusema machache na kumpa mtu mmoja wetu atufanyie sala kabla hatujaondoka. Caleb Amaswache coordinator wa eneo hili.

Caleb Amaswache: Asante sana wananchi wote wenye wako hapa na ma-commissioners, na wale wenzangu wenye wametoka kwa Commission, vile mmesikia wametembea kutoka Pwani, Central Pwani na Western imekuwa ya mwisho, na vile wamesema tena sio mwisho kuja, baado watakuja tufanye provincial meetings.

Langu ni kuwapa wananchi wa Kabras ya chini asante, kwa kuja kwa wingi. Nimeona record yetu hapa ni nzuri kwa kutoa maoni yenu. Commissioners, just one minute before I call the principal to close the meeting. Honourable Angatia I recognize your presence, you are a leader and an opinion leader in this region, please say something.

Honourable Angatia: Asante sana kwa hiyo nafasi kwa niaba ya watu wa area hii, na watu wa Malava kwa jumla, nitawarudishieni wana commission wote, ma-commissioner na staff wao asante kubwa sana; kwa kutupa nafasi ili tusema yale ambayo tumeweza kusema. Tunajua ya kwamba kazi ya katiba ni kazi ngumu, na hii ni mara ya kwanza hii kufanywa katika Kenya; kila mtu ana-tarajia ya kwamba hawa ni wataalam kwa sababu wengi katika nchi hii kuna watu na wale ambaye hawajasoma hawaelewi katiba inaweza kuandikwa namna gani, lakini nyinyi kama wataalam. Na ile msaada mumepata kutoka kwa wananchi, na wataalam wengine tuna hakika na tuna hamu tunatarajia katiba nzuri, ambae inaweza kutuongoza katika shughuli zetu za nchi hii.

Mumekuwa misunderstood ya kwamba katiba itatoa umaskini, ugonjwa, ujinga, sasa hiyo katiba Itatuongoza kwa shughuli za hizo sectors kujaribu kutengeneza mambo yetu.

Lakini katiba peke yake, na hao wazee na staff wao wakati watatupa katiba mpya hawatakuwa wametoa hayo mambo yote, watakuwa wametupa mwongozo. Na katika Kenya miongozo ya kuandikwa ya kufikiriwa, yakutekelezwa na ma-commission ni nyingi tena nzuri sana. Shida imekuwa tu utekelezaji. Mambo yanaweza kutengenezwa na yawe mazuri yaandikwa, lakini watakayoitimiza ndio wanatulet down. So we just want to wish the commissioners every-success wafanye kazi yao waridhike hata sisi turidhike, baadaye watatuwachia itakuwa ni sisi tutailinda namna gani. Sheria iko katika nchi, mambo yako katika nchi hii imeandikwa mazuri, lakini sisi Wakenya wenyewe tumeshindwa namna ya kuwatekeleza.

Jambo ambalo ninajua ni ngumu sana kwa commissioners, kama inawezekana kumshawishi Mkenya aitekeleze haya mambo. Kama mnaweza kuwa na clause katika katiba ambayo Inaweza kuwafanya watu wafanye wajibu wao ingekuwa kitu kuzuri sana. To cheer, people to urge people to be committed, to be patriotic kufanya hiyo kazi. Sijui katiba inaweza kutufanyia

nini ikiwa mngetuletea hiyo, itakuwa mume leta mambo ya ajabu katika nchi hii. Na tutakuwa na maendeleo, tutaleta maendeleo upesi sana. Sitaki kuwapa lecture ingine, sisi tuko tuna furaha tumepata nafasi, najua watu wengine hata hawaelewi katiba ndio nini, kwa hivyo wengine ambao labda wangependa kuwa hapa, hawakuweko. Lakini wale walikuja ndio wale walikuja ndio wale wale walitaka kusema kitu ndio wakazungumza na wakafanya hii kazi kwa niaba ya wengine. Bwana Amaswache sitaki kuongea sana, umejua mimi ni mwalimu na tena mwanasiasa naweza kuongea mpaka watu watachoka. Asanteni sani kwa niaba ya wananchi nitawashika mikono(?) asante sana kuja kututembelea, asante sana na mambo mazuri mumetufanyia, asante sana commissioners.

Caleb Amaswache: Mnajua commissioners why I called honourable Angatia is that my experience in Lugari constituency, is that the area Member of Parliament never attended any of our sessions, instead the former MP Nabwera was there he attended the session, Apili Wawire came and he gave a memorandum and gave his views. In Malava the MP has not attended any of the sessions here, that I was surprised I have seen honourable Angatia here, I saw honourable we Rangai in Matete. So that is why I am saying that may be the Former MPs we replaced are more interested in this constitution and the present MPs. Sina

Mengi, mwalimu walisema wewe ndio utakuja kutufungia, wewe ndie utawaita Omshali, atuombe halafu tufunge kikao. Welcome mwalimu.

Isiah Luchiko Kakai: Isiah Luchiko Kakai:(?) tena kwa niaba ya jamii ya shule ya upili ya Shamoni, commissioners waliofika siku ya leo, na wageni wetu walioko(?) ninayo mwenzangu mwalimu mkuu wa shule ya msingi(?) kuna wengine wengi wamekuja nasema asante sana kwa(?) katika hali hii muhimu.

La pili, nitataja yule ambaye atatuongoza katika maombi na si mwingine basi ni huyu mzee ambaye amejulikana Kiba Kimau Kibe nadhani hakuwa anatarajia kutuongoza katika maombo lakini vile alivyo ni koingozi wa kanisa.....(?) na ningependa kumpa nafasi hii(?) tunapotoka hapa tunaomba ma-commissioners wapitie katika afisi yetu kidogo tu lakini.....(?)

Kiba Kimau Kibe: Prayer Asante sana nafikisha(?) pamoja na officers wote waliofika hapa. Kwa jina Safina W. mwongozo wa(?) wetu kufika hapa kutueleza(?) na kwamba sisi tumepata maneno mingi ambayo hatukujua temejua kwa jina Safi na.....(?) utuongoze watu wetu wakurudi nyumbani waende vizuri, wamalaika wa Mungu utuongoze hawa wazee wakirudi

nyumbani.....
.....(inaudible) Amen.

Isiah Luchiko Kakai: Asante sana Pastor.

The end